# Nipashe

Jumamosi Mei 1, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580567

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**DC** anayedaiwa kutishia kuua ahojiwa polisi

UKURASA 3



**Macho**, masikio ya wafanyakazi kwa Rais leo

UKURASA 4



Lingard akataa kurudi Man Utd

UKURASA 20

# SAMIA HATABIRIKI


- **Aingiza** sura mpya Sekretarieti CCM, aahidi kuvalia njuga kero, Nyalandu arejea 'nyumbani'... *Endelea ukurasa 2 & 4*



Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.



Naibu Katibu Mkuu wa CCM Bara, Christina Mndeme



Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

## Utouh afichua hoja nyeti Ripoti ya CAG

UKURASA 3

**MICHEZO** NI SIMBA VS KAIZER CHIEFS MABINGWA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia hatabiriki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HATABIRIKI! Ndivyo unavyoweza kusema, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuibuka na sura mpya kwenye Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kama ilivyokuwa katika kupendekeza jina la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, na uteuzi wa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, jana Rais aliibuka na majina yasiyotarajiwa ya makada wa CCM wanaochukua nafasi ya Katibu Mkuu na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho.

Muda mfupi baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM na kuuhutubia mkutano mkuu wa chama hicho jijini Dodoma, Halmashauri Kuu Maalum (NEC), ilimpitisha Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo, kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, akichukua nafasi iliyoachwa wazi na Dk. Bashiru Ally.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uamuzi wa kikao hicho cha NEC jana, aliyekuwa Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Humphrey Polepole, alisema kikao hicho chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia, imeridhia kwa kauli moja Sekretarieri mpya ya chama hicho iongozwe na Chongolo.

"Kikao hiki maalum kimeitishwa na Mwenyekiti wetu mpya na kazi ilikuwa moja, kuitizama sekretarieti ambayo ndiyo chombo cha utendaji kwa sababu kila tunapopata mwenyekiti mpya huwa tunapata watenda kazi,"alisema.

Polepole alisema kazi ya msingi ilikuwa ni kuitangaza sekretarieti na kujaza nafasi na kupanga safu ya uongozi katika chama.

"Kama mnavyojua ndani ya chama mtu mmoja kofia moja, kama mnavyojua mimi viongozi wa chama walinipeleka kuwa mbunge na Mwenyekiti wa Bunge kusukuma kazi ya chama kule, hivyo nafasi yangu itachukuliwa na Shaka Hamdu Shaka, kama mnavyojua ana uzoefu mkubwa ndani ya chama," alisema.

Wajumbe wengine wa sekretarieti ni Naibu Katibu Mkuu kutoka Zanzibar anaendelea na nafasi yake Abdallah Mabodi huku Tanzania Bara akiteuliwa Christina Mndeme ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, akichukua nafasi ya Rodrick Mpogolo ambaye atapangiwa majukumu mengine ya kitaifa.

Pia, Makatibu wa NEC wanaoshughulikia Fedha na Uchumi (Frank Hawasi), Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (Ngemela Lubinga), Oganaizesheni (Maudline Castico) anachukua nafasi ya Pereira Silima ambaye pia atapangiwa majukumu mengine.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais, Samia Suluhu Hassan, akipokea Tuzo ya Heshima kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT) Taifa, Gaudensia Kabaka, baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti katika Mkutano Mkuu Maalum, jijiji Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# JKT yawaita vijana kambini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limewataka vijana waliochaguliwa kujiunga na kambi zake kwa ajili ya mafunzo ya kujitolea kwa mwaka 2020/21, kuripoti kwenye kambi walikopangwa.

Hata hivyo, nafasi hizo ni kwa vijana waliorejeshwa nyumbani Februari mwaka huu kutokana na sababu ambazo hazikuainishwa na jeshi hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkuu wa JKT, Meja Jenerali, Charles Mbuge (pichani), Kaimu Mkuu wa Utawala wa JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema vijana wanaotakiwa kuripoti katika kambi za JKT ni wale waliokuwa wamepangiwa hapo awali ambao ni wa elimu ya darasa la saba na kidato cha nne.



Kanali Mabena alisema vijana hao wanatakiwa kuripoti kambini kuanzia Mei 7 hadi Mei 14, mwaka huu huku wale wenye elimu ya kidato cha sita, ngazi ya cheti, stashahada, shahada na wale wenye taaluma ya uhandisi wakitakiwa kusubiri hadi utaratibu mwingine utakapotangazwa.

"Wale wa kidato cha sita, ngazi ya stashahada, shahada na wenye taaluma ya uhandisi wanatakiwa kuendelea kusubiri mpaka utaratibu mwingine utakapotangazwa," alisema.

Alisema vijana hao wataendelea na utaratibu wa kujifunza stadi za kazi ili kuwafundisha kwenda kujitegemea baada ya kuhitimu mafunzo hayo.

Kanali Mabena alisema kwa vijana wanaotarajiwa kuhitimu kidato cha sita mwaka huu, watakwenda kwenye mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria.

"Tayari ufuatiliaji wa majina ya wanaoshiriki kwa mujibu wa sheria umeanza," alisema.

# Rais Samia aahidi kutenda haki CCM

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku akiahidi kuendeleza mfumo thabiti wa uwazi, kutoa haki katika michakato ya uchaguzi wa ndani ya chama na wa kupata wawakilishi katika nafasi za kitaifa.

Mbali na hilo, ameahidi kusimamia misingi ya chama, kuendeleza utamaduni wa kujitathmini, kujisahihisha na kufanya mabadiliko kwa lengo la kukiimarisha chama. Kwenye mkutano huo uliohudhuriwa na wanachama 1,876 jana, Rais Samia alichaguliwa kwa kishindo kwa kupata kura zote 1,862 za wajumbe 1,862 waliopiga kura.

Akizungumza baada ya kutangazwa kuwa Mwenyekiti mpya wa CCM, Rais Samia alisema anakwenda kujenga imani kwa wananchi na kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea duniani.

"Ninajua jukumu mlilonipa la kuwa mwenyekiti siyo rahisi, ila nitaweza, sababu za kwaza ni kwamba CCM inaongozwa na kanuni, taratibu na katiba ambayo ninaahidi nitaifuata.

"Nimekuwa mwanachama wa CCM kwa miaka 34, nina uzoefu wa miaka 20 ndani ya vikao vikubwa vya kufanya uamuzi. Ninayajua yanayoamuliwa ndani ya chama. Ninajua ndani ya CCM kuna umoja, ushirikiano na mshikamano," aliahidi.

Rais Samia pia aliahidi kujikita katika kuwahamasisha viongozi wenzake katika ngazi zote ndani ya chama kupitia kwa kina sera na miongozo inayoelekeza itikadi, imani, mwelekeo na majukumu ya chama.

Alisema lengo kuu ni kuangalia masuala yanayofaa kwa hali na mwenendo wa dunia kwa wakati wa sasa kwa lengo la kusonga mbele.

"Pia nitasimamia maadili, kanuni za chama ili kujenga misingi ya wanachama wanaotambua wajibu wao kwa chama na taifa lao," alisisitiza.

### UTATUZI WA KERO

Rais Samia pia aliahidi kutatua vikwazo mbalimbali vinazowakabili wanachama wa CCM.

Kwanza, Rais Rais aliahidi kutatua kikwazo cha uhaba wa vitendea kazi, akisema: "Kwa mfano baadhi ya mikoa na wilaya, viongozi hawana vyombo vya usafiri, jambo ambalo linadumaza shughuli za chama ndani na nje. Ninaahidi kwenda kutatua."

Pili, Rais Samia aliahidi kutatua kero ya maslahi duni kwa watumishi wa chama.

Tatu, aliahidi kutatua kero ya malimbikizo ya madai ya stahiki za watendaji wa chama yakiwamo malimbikizo ya madai ya uhamisho pamoja na kustaafu.

"Changamoto zingine tutazitatua wenyewe, chama kukaa pamoja, tujitathmini na tujirekebishe ili tuimarishe itikadi na imani yetu," alisema.

Rais Samia alisema tangu kuanzishwa kwa CCM kumekuwa kukifanyika mabadiliko ya kimuundo na kiutendaji, ikiwamo ama kuanzisha au kufuta baadhi ya nafasi ndani ya chama.

Alisema chama kilifanya mabadiliko kwa kupunguza au kuongeza wajumbe wa vikao vya uamuzi, lengo likiwa ni kuongeza ufanisi na kupunguza gharama ndani ya chama.

Rais Samia alisema: "Pia tulifanya uhakiki na kurejesha rasilimali za chama, tulipitia upya mikataba mbalimbali ya biashara na uwekezaji na kuanzisha mfumo wa kieletroniki, ikiwamo usimamizi wa mali na rasilimali za chama," alikumbusha.

Alisema lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha mapato na chama yanadhibitiwa.

Rais Samia alibainisha kuwa kutokana na hatua hizo, chama kimefanikiwa kuongeza mapato na jumuiya zake kutoka Sh. bilioni 50 hadi Sh. bilioni 60 sawa na ongezeko la asilimia 21.8

Pia alisema thamani za mali za chama zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 120 hadi Sh. trilioni moja. Alisema CCM kwa sasa ina wanachama wapatao milioni 12, hivyo kinapaswa kuna na jukumu la kuhakikisha kinakuwa sauti ya Watanzania na kinahusika moja kwa moja katika kuhamasisha maendeleo ya nchi sambamba na kusimamia serikali

"Ninatoa angalizo kwa viongozi wetu wa CCM ngazi mbalimbali, kuacha kuwa sehemu ya kutengeneza migogoro baina ya watendaji wa serikali na wananchi, bali tuwe daraja la kuwasaidia wananchi katika maeneo yetu kupata huduma zinazostahiki," alionya.

Aliwataka wanachama wa CCM kuwa na wajibu wa kuhakikisha serikali inatekeleza ahadi ilizozitoa, kwamba ushindi wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 utaletwa na namna ilani itakavyotekelezwa kwa Watanzania.

## HABARI KITAIFA

# Utouh aibua hoja nyeti Ripoti ya CAG

**Na Sanula Athanas**

TAASISI ya WAJIBU inayoongozwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) wa zamani, Ludovick Utouh, imefanya uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2019/20 na kuibua hoja nyeti katika Sekta ya Uwekezaji nchini.

Katika uchambuzi wake huo, taasisi hiyo imeainisha kupungua kwa asilimia 48 ya miradi ya uwekezaji na biashara nchini iliyosajiliwa kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC) na hivyo kupunguza ajira kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi waajiriwa 32,115 mwaka 2019/20.

Kiwango hicho cha kuporomoka kwa ajira katika miradi ya uwekezaji nchini ni takribani nusu ya ilivyokuwa mwaka 2015/16.

Akiwasilisha mada kuhusu Uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2019/20 wakati wa mjadala wa asubuhi ulioandaliwa na Policy Forum jijini Dar es Salaam jana, Utouh alibainisha kuwa dosari hiyo katika uwekezaji na biashara ni sehemu ya kiini cha kilio cha uhaba wa ajira nchini.

Utouh ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alibainisha kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21, mbali na mambo mengine, unaitaka serikali kuhamisha, kuwezesha na kuratibu uwekezaji, mabadiliko ya teknolojia, viwanda na biashara.

Alibainisha kuwa hali hiyo ilichangiwa na kutokuwa na mazingira rafiki kwa wawekezaji, akibainisha kuwa Tanzania iko nafasi ya 141 kwenye orodha ya nchi 190 kwa vigezo vya mazingira rafiki kwa uwekezaji.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa Tanzania imeshuka kwa asilimia nane katika kutengeneza mazingira rafiki kwa wawekezaji katika kipindi cha miaka mitano (2015-2020).

Alisema hali hiyo pia imechangiwa na TIC kutotoa huduma zote za kiuwekezaji (one stop centre), akibainisha kuwa inatoa huduma nne tu kati ya 11 zinazotakiwa.

"Kuna ucheleweshaji wa mrejesho wa maombi ya uwekezaji katika mamlaka husika. Vigezo vya kimataifa vinataka iwe ndani ya siku 14 lakini uhalisia uliopo nchini ni siku 182 hadi 675," alisema.

Alibainisha kuwa Tathmini ya Athari za Mazingira inayotekelezwa na NEMC nayo imekuwa ikichukua muda mrefu kukamilika, ikiripotiwa na CAG kuchukua siku 95.

Vilevile, alinyooshea kidole vikwazo vya uhaba wa bajeti, akibainisha kuwapo upungufu wa Sh. 45 bilioni (asilimia 49 ya mahitaji) katika mwaka wa ukaguzi na uhaba wa watumishi (asilimia 35 ya mahitaji ya watumishi 513).

Alionya kuwa hali hiyo ikiendelea, uwajibikaji utapungua miongoni mwa watendaji wa serikali, akikumbusha namna alivyoibua sakata la uwapo wa watumishi hewa serikalini lakini hatua hazikuchukuliwa mapema.

Utouh alisema utekelezaji wa mapendekezo yake ulifanyiwa kazi na Hayati Rais John Magufuli mwaka 2016, serikali ikifanikiwa kuokoa takribani Sh. bilioni 19 zilizokuwa zinapotea kulipa watumishi hewa kila mwezi.

"Mwaka 2012 nilihoji kuhusu mmiliki wa PRIDE. Mwaka 2017/18 CAG (Prof. Mussa) Assad akahoji kuhusu mmiliki wa PRIDE, 2018/19 CAG (Charles) Kichere akahoji suala hilo hilo. Leo mmiliki amekimbilia Amerika ameacha matatizo makubwa," alisema.

Utouh pia alinyooshea kidole mashirika na taasisi za umma 30 kujiendesha pasi na uwapo wa bodi za wakurugenzi, akibainisha kuwa kati yake, 20 zilijiendesha kwa chini ya mwaka, tisa kwa zaidi ya mwaka na moja kwa zaidi ya miaka miwili bila kuwa na bodi.

Alisema uchambuzi wa taasisi yao pia umegusa mifumo ya kiteknolojia (ICT) ambayo serikali inaitumia kwenye maeneo mbalimbali, akisema kuna shida ya kutokuwa na muunganiko wa kiutendaji.

"Jiulize kwanini leo taarifa unazotakiwa uwasilishe kupata kitambulisho cha uraia ni zilezile unazopaswa kuwa nazo ili kupata hati ya kusafiria? Kwanini mifumo ya taasisi hizi mbili (NIDA na Uhamiaji) isifanye kazi kwa pamoja?" Utouh alihoji.

Mbali na hayo, Utouh pia aligusia kutokumika kwa miradi iliyokamilika, marejesho duni ya fedha za mikopo inayotolewa na halmashauri kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, rushwa na ufisadi, athari za corona pamoja na rushwa na ufisadi.

"Serikali ifanyie kazi mapendekezo ya CAG na kamati husika za Bunge ili kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji miongoni mwa watendaji wa umma.

"Serikali pia ifanyie kazi dosari zilizoibuliwa kwenye mifumo ya ICT, kuchukua hatua dhidi ya rushwa na ufisadi na kurekebisha vikwazo katika uwekezaji na biashara vilivyoibuliwa," Utouh alihitimisha.

| Jina | 2015/16 | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|---|---|---|
| Miradi iliyosajiliwa | 420 | 352 | 274 | 272 | 219 |
| Thamani (Dola mil.) | 7,716.39 | 2,777 | 2,285 | 2,577.57 | 1,853.47 |
| Ajira zilizozalishwa | 63,223 | 26,051 | 33,702 | 48,102 | 32,115 |

*Kupungua kwa miradi mipya iliyosajiliwa TIC kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2020/21.* ***CHANZO: Taasisi ya WAJIBU Aprili 30, 2021***

### VIWANDA VYA MASHIRIKA

Utouh pia alizungumzia kuchelewa kutolewa uamuzi wa serikali juu ya kuanza kufanya kazi kwa viwanda vilivyojengwa na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Alivitaja viwanda hivyo kuwa ni pamoja na cha dawa cha mkoani Simiyu, cha chai cha Lushoto mkoani Tanga na cha sukari cha Mkulazi mkoani Morogoro.

Utouh, aliyekuwa CAG kwa miaka nane kuanzia mwaka 2006 hadi 2014, alisema kuwa baada ya kuichambua Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20, wamebaini bado utekelezaji wa mapendekezo ya CAG uko chini.

# DC ahojiwa madai kutishia kuua

**Na Thobias Mwanakatwe**

JESHI la Polisi Mkoa wa Songwe, limeanza uchunguzi tuhuma za Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Samuel Jeremiah, kuhusu kumtishia kumuua Mbunge wa Songwe (CCM), Philip Mulugo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili jana, alisema jeshi hilo limeanza uchunguzi na tayari limeshamwita na kumhoji Jeremiah.

"DC anahojiwa na yule aliyetuhumu (mbunge) naye anahojiwa. Hakuna aliyeshtaki isipokuwa taarifa kama hii usisubiri mpaka mtu ashtaki. Tuhuma kama hizi kwa viongozi kama hawa wa serikali lazima jeshi lichunguze ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Kamanda Kyando alisema baada ya uchunguzi kukamilika na ikionekana kuna jinai sheria itachukua mkondo wake na kama ikibainika hakuna, hatua nyingine zitachukuliwa ili kumaliza suala hilo.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Mulugo alimtuhumu mkuu huyo wa wilaya kwamba amemtishia kumuua.

Mulugo alisema hayo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, kwenye kikao cha wadau wa zao la ufuta kilichojumuisha watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, madiwani, wanunuzi wa zao hilo, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wakulima.

Mbunge huyo alieleza sababu za kudai kutishiwa na DC huyo kuwa ni pamoja na kumfuatilia mkuu huyo wa wilaya kuhusu fedha zinazotolewa na wawekezaji wa maendeleo wilayani zikiwamo kampuni kubwa za uchimbaji wa madini na wachimbaji wadogo.

Pia alidai kuwa sababu nyingine ni kutokana na kufuatilia fedha za michango ya wananchipale wanapoamuriwa kuchangia miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya cha Mbuyuni.

Mulugo pia alisema vitisho dhidi yake pia vimetokana na yeye (mbunge) kuwa mstari wa mbele kuwatetea wakulima wa ufuta ambao walisema hawako tayari kwa sasa kupeleka mazao yao kuuza kwa mfumo wa stakabadhi ghalani uliokuwa umetangaza na serikali ya wilaya.

Madai hayo ndani ya mkoa ni ya pili baada ya lile la Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi, Hanji Godigodi, kudai kutishiwa kuuawa na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Songwe, Henerico Mkola, na taarifa za tukio hilo kuripotiwa kituo cha polisi Vwawa na kupewa RB namba MBZ/IR/200/2021.


**DABRI AUCTION MART COMPANY LIMITED**

DABRI AUCTION MART COMPANY LIMITED

*We are dealing with Debt collection, General Auctioneers & Commission Agent*

Email: Dabriauctionmart@yahoo.com Website: dabriauctionmart.co.tz P.o.Box 664 Dar es salaam
Location: Mwananyamala Phone: +255 657 507050/ +255 713 401175

Sisi D**abri Auction Mart Company Limited** kwa idhini tuliyopewa na Benki ya **Letshego** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa tangaza la mnada wa hadhara wa kuuza mali za mdaiwa/mdhamini tajwa hapo chini kama vilivyoorodheshwa.Minada itafanyika katika maeneo dhamana zilipo.

| S/N | JINA LA MKOPAJI | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | ENEO ILIPO DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 110128 KIWANJA NAMBA 249 KITALU NAMBA 6 | KIBADA,MANISPAA YA TEMEKE | TAREHE 07/05/2021 SAA 5:00 ASUBUHI |
| 2. | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | QUEEN LINGTON SAKANYAGA | HATI NAMBA 121999 KIWANJA NAMBA 135 KITALU NAMBA 32 | BUYUNI,MANISPAA YA ILALA | TAREHE 07/05/2021 SAA 9:00 ALASIRI |

**MASHARTI YA MNADA.**
1. Mnunuzi atalazimika kulipia 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada na salio la 75% litalipwa ndani ya siku 14 tangu siku ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipia salio ndani ya siku 14, atakua amepoteza haki yake ya malipo ya 25% na dhamana itauzwa tena.
3. Gharama zote kuhusu kubadilisha jina na umiliki wa dhamana zitakua juu ya mnunuzi.

Kwa maelezo zaidi fika kwenye ofisi zetu zilizopo Mwananyamala au wasiliana nasi kwa namba za simu 0626932958 na 0621477104



**COFFEE HUB COMPANY LIMITED**
**Cheti cha usajili namba 138836932**
**Sheria ya mahakama.2002**
**(KIFUNGU 334(1)**

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha Coffee Hub Kampany Limited(kampuni),yenye usajili namba 138836932, kilichofanyika tarehe **09 April 2021** azimio maalumu lilipitishwa:
1. Kufuatana na kifungu 331 (1)(b) cha sheria ya makampuni ya 2002,kuwa kampuni ifutwe kwa hiari na
2. Wanahisa wamemteua Linda Allan Mwambete wa mikumi House,368 msasani road,oysterbay SLP 9673, Dar Es Salaam,Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku thelathini (30).

Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

Linda Allan Mwambete
Liquidator
For SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED



**KUPOTEA KWA CHETI**



**SHUMBANA RAMADHAN TAUFIK** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.326/72** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **LUMUMBA SEKONDARI** mwaka 1986. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/222328/2020.**



**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**NASSOR HEMED SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T. 920 BHC** aina ya TOYO. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.
Taarifa ya Polisi **KAH/TR/RB/179/2021.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**HATI YA KIAPO**

Mimi **FRANCIS BONIFES TUPA** wa S.L.P 42 Nachingwea Mkristo mtu mzima na akili zangu timamu nathibitisha haya yafuatayo:-
1. **KWAMBA** mimi ni msimamizi wa mirathi Na. 37/2012 ya marehemu **BONIFES TUPA.**
2. **KWAMBA** marehemu alikuwa akimiliki nyumba iliyopo katika kiwanja Na. 5 kitalu "C" Kisosora Tanga.
3. **KWAMBA** katika kukusanya mali za marehemu nimegundua hati ya nyumba hiyo imepotea na jitihada ya kuitafuta imeshindikana. Nimefika kutoa taarifa polisi. **TAN/RB/222897/2021.**
4. KWAMBA kwa kiapo hiki ninaomba Afisa Ardhi kutoa Hati (Toleo) ya nyumba hiyo kwa jina la marehemu **BONIFES TUPA** kwa sababu ile ya awali imepotea.

Ninathibitisha kwamba niliyoyatamka hapo juu ni kweli tupu kadri ninavyofahamu sheria ya viapo.

**MBELE YA…MR. KOMBO**
**CHEO…HAKIMU**

FRANCIS BONIFES TUPA



**SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED**
**Cheti cha usajili namba 125531**
**Sheria ya mahakama.2002**
**(KIFUNGU 334(1))**

**MAAMUZI YA HIARI YA WANAHISA KUFUNGA KAMPUNI**

Umma unafahamishwa kuwa katika kikao cha sauti ya uzima Radio Kampany Limited(kampuni),yenye usajili namba 125531,kilichofanyika tarehe 09 April 2021 azimio maalumu lilipitishwa:
1. Kufuatana na kifungu 331 (1)(b) cha sheria ya makampuni ya 2002,kuwa kampuni ifutwe kwa hiari na
2. Wanahisa wamemteua Linda Allan Mwambete wa mikumi House,368 msasani road,oysterbay SLP 9673, Dar Es Salaam,Tanzania kuwa mfilisi wa kampuni

Umma na wahusika wanafahamishwa kupeleka madai yao kwa usaili ndani ya siku tghelathini (30).
Maombi yote yatayopelekwa baada ya siku 30 kuisha hayataandikishwa.

Linda Allan Mwambete
Liquidator
For SAUTI YA UZIMA RADIO COMPANY LIMITED



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya simu:WARAKA
Simu: 2548570 au 2502805
Telefax 2124576
Telex 2271
Unapojibu tafadhali taja:

Baraza la Ardhi na Nyumba
S.L.P. 5058,
TANGA.
17/11/2020

**YAH: SHAURI NA 6 LA 2021**
**SAID HAMADUN BAKARI……………………………MDAI**
**DHIDI**
**MGENI ATHUMAN RIKO, RAHMA ABDALLAH, ESTHER MAGEMBE, RAMADHANI SAID HABIBU, AISHA MOHAMED MAUMBA, HUSSEIN MBWANA MWAKIFAMBA……...WADAIWA**

**KWA: RAHMA ABDALLAH RIKO, ESTHER MAGEMBE, RAMADHANI SAID HABIBU, AISHA MOHAMED MAUMBA, HUSSEIN MBWANA MWAKIFAMBA - POPOTE WALIPO**

Mwombaji aliyetajwa hapo juu amefungua shauri dhidi yako katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wliya ya Tanga.
Unaarifiwa kufika. Mnamo tarehe 20/5/2021 saa tano (05:00) asubuhi ambapo shauri hili litakuja kutajwa. Hivyo basi unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, Shauri hili litasikilizawa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI. Hii imetolewa kwa mkono wangu na mhuri/Lakiri ya Baraza hili leo tarehe 23/4/2021.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TANGA**



Wafanyakazi wa mgodi wa dhahabu wa Barrick North Mara, wakiendelea na shughuli ya maandalizi ya mabanda ya maonyesho katika viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza jana, kwa ajili ya maadhimisho ya sikukuu ya wafanyakazi (Mei Mosi), ambayo kitaifa yanafanyika mkoani Mwanza leo. **PICHA: ROSE JACOB**

# Macho na masikio Mei Mosi Mwanza

**Mwandishi Wetu,** MWANZA

MACHO na masikio ya wafanyakazi nchini yanaelekezwa Mwanza ambako maadhimisho ya kitaifa ya Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yanafanyika.

Kiu hasa ya wafanyakazi ni kutaka kujua kama Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye anatarajiwa kuwa mgeni rasmi, atatangaza neema ya kupandishwa kwa mishahara.

Hali hiyo inatokana na ukweli kwamba kwa zaidi ya miaka mitano, mishahara ya wafanyakazi haijawahi kupandishwa,

Wakati hayo yakitarajiwa. Maandalizi ya sherehe hizo zinazofanyika katika Uwanja wa CCM Kirumba, yamekamilika huku uongozi wa mkoa ukiwahakikishia usalama wageni wote wanaoshiriki maadhimisho hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, jana alisema wamejipanga ili kuhakikisha sherehe zinafanyika kwa amani. Aliwataka wananchi na wafanyakazi wa serikali na sekta binafsi kujitokeza kushiriki maadhimisho hayo.

Mongella alisema siku ya Mei Mosi ilianzishwa na wafanyakazi waliokuwa wakidai haki na maslahi yao katika maeneo mbalimbali duniani na kwamba kuanzia hapo wafanyakazi wamekuwa wakiadhimisha.

Kwa upande wake, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne Muliro, akitangaza hali ya usalama, alisema mtu yeyote atakayejaribu kuvunja amani, usalama ama kufanya uhalifu wowote katika kipindi hiki na kijacho atashughulikiwa.

Alisema usalama umeimarishwa na kwamba kila mtu atakayefika jijini Mwanza ataweza kukaa kwa amani hadi atakapoondoka.

# Nyalandu arejea CCM

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa zamani wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu na kigogo mwingine wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamerejea Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakidai kuguswa na maono ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza jana baada ya kupewa nafasi na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia, kuzungumza kwenye mkutano mkuu maalum, Nyalandu alisema ana anawashukuru wajumbe kwa kukubali kumpokea na kumsamehe na kumruhusu kurejea tena nyumbani.

"Kwa hakika, Mwenyekiti hakuna furaha izidiyo furaha ya mtoto arejeapo nyumbani na huko nyumbani haulizwi tena kule ugenini nyumbani unarudi lini? Ni swali ambalo nimekumbana nalo muda mrefu.

"Nukuu katika kitabu kizuri cha Zaburi 137:1-4 ..... Mheshimiwa Mwenyekiti hakika nchi ya ugenini wimbo hauimbiki, Mzee Lowasa, Sumaye, Slaa hawa ni mashuhuda, wachache kati ya wengi kwanini wimbo wa bwana hauimbiki katika nchi ya ugenini.

"Watanzania wameiona nyota yako, wameguswa na kujaa na furaha na matumaini kwa kuinuliwa kwako kwa kuwa Mungu alikuandaa kuwa kiongozi wa taifa hili tangu misingi ya ulimwengu,"alisema.

Nyalandu alisema kuwapo kwake kwenye mkutano huo ni kielelezo cha Rais Samia kuungwa mkono na Watanzania wote.

"Mama tuma neno lako likaponye wale ambao wameumia na kuhuwisha ndoto za Watanzania wote, Mama na Rais na Mwenyekiti wetu ukaitwe heri na shujaa wa mioyo ya Watanzania,"

"Ukaongeze tabasamu katika nyuso za Watanzania wote kwa kuyaenzi na kuyaendeleza matamanio yao juu ya uimara wa taifa lao unalo liongoza,"alisema.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kusini Mkoa wa Lindi, Suleiman Luwongo, alisema alihisi kuwa na upungufu kukaa nje ya chama hicho.

"Nimeamua kurudi nyumbani, nilikuwa ndani ya CCM na niliondoka ndani ya CCM, kadri unavyokuwa nje ya CCM unajihisi mwenye upungufu, ninakuja kwenu kwa wajumbe wa mkutano mkuu na mimi leo (jana) nimeingilia hapa hapa ambapo Rais Samia amekuwa Mwenyekiti wa kwanza mwanamke wa CCM," alisema.

Aliahidi kumuunga mkono kwa asilimia 100 Rais Samia na amerudi CCM ili kuendeleza maendeleo yanayofanywa na CCM.

Akizungumza baada ya kuwapokea, Samia aliwakaribisha CCM huku akisema wapo wengi lakini kwa jana zawadi yake kwa wajumbe wa mkutano huo ni hiyo.


NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU



Mei Mosi 2021
Siku ya Wafanyakazi Duniani

*"NHC tunaendeleza Taifa katika Ujenzi Bora wa Nyumba na Makazi"*





**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) tunaungana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan na Watanzania wote kusherehekea sikukuu ya wafanyakazi duniani**

**Mei Mosi 2021**

Sanduku la Posta 2977, Dar Es Salaam | Simu: +255 22105002-6 | Barua Pepe: dg@nhc.co.tz | Tovuti: www.nhc.co.tz

**HABARI KITAIFA**

# Raia Iran kizimbani Lindi tuhuma kilo 800 Heroine

**Na Waandishi Wetu**

RAIA saba wa Iran wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Lindi wakikabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi yakiwamo mashtaka mawili yanayohusiana na kusafirisha kilo 859.36 za dawa za kulevya aina ya Heroine na Methamphetamine.

Washtakiwa hao ni: Jan Miran (42), Issa Ahmad (30), Amir Kasom (35), Salim Baluchi (20), Ikibal Mohammad (22), Mustapha Barksh (20) na Jawid Mohammad (19).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Maria Bantulayne.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Joseph Maugo na Juma Maige.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa katika shtaka la kwanza, Aprili 23, 2021, katika eneo la Bahari ya Hindi, Mkoa wa Lindi, washtakiwa walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine kilo 504.36.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na mahali pa tukio la kwanza, washtakiwa wote walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya Methamphetamine kilo 355.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kutoka na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi bila kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) au upelelezi utakapokamilika itahamishiwa Mahakama Kuu.

Hakimu Bantulayne alisema kesi hiyo itatajwa Mei 14 mwaka huu na washtakiwa walipelekwa mahabusu.

Imeandikwa na Hellen Mwango(Dar) na Said Hamduni (Lindi)



Viongozi mbalimbali pamoja na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, wakifurahia wakati wa mkutano huo. **PICHA YA MTANDAO**

## Askari JTWZ mbaroni tuhuma za kumuua mkewe kisa wivu mapenzi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamshikilia Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Praiveti Godfrey Magiladi, kwa tuhuma za kumchoma kisu hadi kufa mke wake Fatuma Salumu.

Magiladi ambaye ni askari wa Kikosi cha Jeshi Namba 36 (36 KJ) anadaiwa kumuua mkewe huyo ambaye alikuwa mkazi wa Mwanalugali Kata ya Tumbi, wilayani Kibaha kwa madai ya kufanya tendo la ndoa nje ndoa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 25, mwaka huu, majira ya saa 4:00 usiku eneo la Mwanalugali. Alisema Fatuma alifariki dunia akiwa njiani kwenda Hospitali ya Tumbi kwa ajili ya matibabu.

Wankyo alisema mtuhumiwa amekamatwa baada ya tukio hilo na mahojiano yanaendelea na upelelezi ukakamilika, atafikishwa mahakamani.

Alisema baada ya kufanya tukio hilo, mtuhumiwa alikimbia na kumwacha mke wake, ambaye sasa ni marehemu, akiwa chini hadi wasamaria wema walipojitokeza na kumchukua kumpeleka hospitalini.

Katika tukio lingine, mwanamke mmoja (jina linahifadhiwa) ambaye alikuwa mfanyabiashara wa pombe za kienyeji aliokotwa akiwa amefariki dunia katika mazingira ya kutatanisha.

Kamanda Wankyo alisema kabla ya kifo, Aprili 25 usiku wa manane akiwa na mama yake mzazi wakitokea katika kilabu chao cha kuuzia pombe, walirudi nyumbani kwa mama yake.

Alisema baadaye mwanamke huyo aliaga kutoka kwa mama yake kwenda kwake na hakufika mpaka alipookotwa pembezoni mwa barabara akiwa amefariki dunia kwa kunyongwa shingo.

Jeshi la Polisi linawashikilia watu 17 wanaohusishwa na tukio hilo ambao wanaendelea kuhojiwa.


## NOTISI / TANGAZO

**NUTMEG AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, MASHOKA AUCTION MART, SUNDI AUCTION MART LTD,TAUSI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEERS AND DEBT COLLECTORS LTD, BEST GROUP LTD, SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadai wa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | TAREHE NA SAA YA MNADA | MAHALI DHAMANA ILIPO |
|---|---|---|---|---|---|
| RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | MWANZA | RWEYEMAMU MENDRAD KABENDERA | KIWANJA TITLE NO. 74288/LO NO 542135/PLOT NO 318 BLOCK "A" | 19.5.2021 /SAA 3:30 NA KUENDELEA | SHILABELA/ NYASHISHI |
| GRACE BARNABAS MASUKA | MWANZA | GRACE BARNABAS MASUKA | NYUMBA | 19.5.2021 /SAA 3:30 NA KUENDELEA | MTAKUJA/USAGARA |
| MARIA DAMAS JOSEPH | MWANZA | A. MARIA DAMAS JOSEPH | A. KIWANJA, PLOT NO 66, BLOCK C | 22.5.2021 | KISHIRI "B" |
| | | B. WABISWA KABOGA KAPUMU | B. KIWANJA, PLOT NO 64, BLOCK C | SAA 3:30 NA KUENDELEA | KISHIRI "B" |
| ALKAD LAURIANI KAZALANI | MWANZA | ALKAD LAURIANI KAZALANI | KIWANJA KILICHOENDELEZWA | 24.5.2021 /SAA 3:30 NA KUENDELEA | KAWEKAMO "B"/MSUMBIJI |
| ANAUFOO FURAEL SAWE | MWANZA | LIGHTNESS BONIPHACE KABEGWE | NYUMBA | 27.5.2021 /SAA 3:30 NA KUENDELEA | BUDUKU/KAHAMA/ |
| FROLIAN ISDORY PONZA | MBAGALA | FROLIAN ISDORY PONZA | NYUMBA | 17/5/2021 SAA 10: 00NAKUENDELEA | MZINGA-MBAGALA |
| EDNA MOSES MTEI | MBAGALA | DONATH JOHN KALEBA/RONATHA J MWANGOSI | NYUMBA | 16/5/2021 SAA 12:00NAKUENDELEA | MTONI KIJICHI |
| GESSINE SESSINE MWIKWABE | MBAGALA | ROSE ALEX KIMARO | NYUMBA | 16/505/2021 SAA 20:00 NAKUENDELEA | KIZINGA- DAR ES SALAAM |
| RASHID SAID MSUYA | BUGURUNI | RASHID SAID MSUYA | NYUMBA | 20/5/2021 SAA SAA 09:00 NAKUENDELEA | MKODONGWA - MBAGALA SAKU |
| ANNA GABRIEL CHUWA | BUGURUNI | MUSSA MAGAMBI KASHID | NYUMBA | 20/5/2021NAKUENDELEA | CHANIKA - NZASA |
| KAJIGILI INVESTMENT COMPANY LIMITED | MBEYA | JOSEPH KAJIGILI MWANDOBOKA | GARI TOYOTA CANTER,T 178 DGQ | 14/5/2021 SAA 10:00 NAKUENDELEA | TABATA ,DAR ES SALAAM |
| VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | STORE NA FREMU ZA MADUKA ZENYE HATI MILIKI | 23/05/2021 SAA 10:00 NAKUENDELEA | MWANJELWA , MBEYA MJINI |
| MWANAHAMISI ATHUMANI LUMAJA/ ELVIS LUYEGO | MBAGALA | MWANAHAMISI ATHUMANI LUMAJA /ELVIS LUYEGO | NYUMBA | 17/5/2021 SAA 10:00 NAKUENDELEA | HONDA VIANZI-MKURANGA |
| STAPHOD CHRISTOPHER SENYE/JUNIOR &ANDREW BUSSINES | MBAGALA | STAPHOD CHRISTOPHER SENYE | NYUMBA | 17/05/2021 SAA 12:00 NAKUENDELEA | MKWALIA-MKURANGA |
| NATHAN MASUMBUKO DANGA | MBAGALA | NATHAN MASUMBUKO DANGA | NYUMBA | 18/5/2021 SAA 12:00 NAKUENDELEA | MKURANGA |
| MANENO MUSSA ISMAIL | MBAGALA | MANENO MUSSA ISMAIL | NYUMBA | 17/5/2021NAKUENDELEA | SANDALI - USALAMA |
| ABDUL RAMADHAN NDAGINE | MBAGALA | MADARAKA MOHAMED MFAUME | NYUMBA | 19/05/2021NAKUENDELEA | MBAGALA CHARAMBE-KIMBANGULILE |
| MUSTAPHA ISSA MNYALU | MBAGALA | MUSTAPHA ISSA MNYALU | NYUMBA | 21/05/2021NAKUENDELEA | KOKOMWANGA |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolotela mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 / 07130774774/ 0754497396
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa namnunuzi bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mikataba mipya ya nyota Ligi Kuu izingatie uhalisia

**KUELEKEA** ukingoni kwa msimu uliopo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni dalili za wazi kuwa msimu mwingine mpya umekaribia.

Kwa sasa Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuingia katika mzunguko wa 28, na hii inamaana kwamba zimebaki raundi sita ili msimu wa 2020/21 ufikie tamati.

Sio Ligi hiyo tu, bali hata Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania pia ziko katika hatua ya lala salama. Timu zinazoshiriki ligi hizo tayari zimeshagawanyika katika makundi matatu ambayo yanaonyesha nafasi ya kila klabu kulingana na pointi ilizovuna katika michezo yote iliyochezwa.

Kundi la kwanza ni la timu zinazokimbizana katika Vita ya kuwania ubingwa, la pili ni lile ambalo linaamini liko katika nafasi salama ambapo hawawezi kipitiwa na panga la kupiga ligi hiyo na kundi la mwisho ni la klabu zinazojiepusha na janga la kushuka daraja.

Kwa maana hiyo,kila mmoja sasa hivi anafahamu vyema malengo yake kuelekea msimu mpya wa mwaka 2021/22 ambao nao hauko mbali na maandalizi yake yanatakiwa yaanze mapema ili kuwa na kikosi imara.

Kwa kuangalia hilo, Nipashe inazikumbusha klabu na wachezaji kufanya mazungumzo yatakayofaidisha pande zote mbili kwa matarajio ya kupata matokeo chanya na tuachane na utamaduni wa kukataa kuuza mchezaji anayetakiwa nje ya Tanzania na kumbakisha nchini kwa dau lenye thamani ndogo. Tayari tumeshaona klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara zimeanza kuingia mikataba mipya na wachezaji wake wa zamani na nyingine zimesajili nyota wapya ili kuimarisha vikosi vyao kuelekea msimu mpya.

Kufanya usajili mapema ndio jambo zuri, lakini mchakato huu ili uweze kuipa timu matokeo chanya ni vyema ukawa na faraja kwa pande zote mbili, hilo likifanyika kwa umakini, tunaamini timu husika itajiweka kwenye nafasi ya kupata ushindi na kufikia kile inachokihitaji.

Nipashe inakumbusha suala la maslahi kwa ajili ya kutaka kuona wachezaji wanapokea mishahara na bonasi wanazostahili na klabu pia inapata matokeo kulingana na uwekezaji walioufanya. Tumeshuhudia klabu nyingi hapa nchini zikiwapa kiasi kidogo cha fedha za usajili wachezaji wazawa na kutoa mamilioni kwa nyota wanaotoka nje ya Tanzania, na uamuzi huu kuleta migongano katika siku za usoni.

Timu inapofanya makosa katika usajili, basi ni wazi huko mbele msamiati wa kutwaa ubingwa katika ligi inayoshiriki au mashindano yoyote huwa ni ngumu au unaweza kusema wanababahatisha.


Nipashe inazikumbusha klabu kuwa makini katika mazungumzo na wachezaji inaowahitaji kwa kuwapa malipo wanayostahili na kwa kufanya hivi watawajenge nyota hao moyo wa kujituma kuanzia mwanzo hadi mwisho wa msimu kwa sababu watakuwa wanazungumza lugha moja.

Kama ambavyo tumeshuhudia baadhi ya wachezaji wetu kutakiwa na timu za nje, hii inaonyesha kwamba Soka la Tanzania na hasa Ligi Kuu Bara imekuwa bora, hivyo ili kulinda mazuri haya yaliyoanza kuonekana, ni wakati wa viongozi kuthamini michango inayotolewa nyota wa hapa nyumbani.

Kuwasajili kwa kuwapatia fedha zinazostahili kulingana na viwango vyao, kutawaongezea morali wachezaji husika na mwisho wa siku kuwa tayari pia kuzitumikia Timu za Taifa ambazo hutegemea wachezaji waliolelewa vyema katika ngazi ya klabu.

Tunawakumbusha ili timu yoyote iweze kufanya vizuri katika msimu inayofuata, huu ni wakati wa kufanya mchakato wa usajili kwa umakini na weledi huku wakiwakumbusha wachezaji kudumisha nidhamu ndani na nje ya uwanja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Siku zote penye nia pana njia

Na Barnabas Maro

**NIA** ni dhamira ya kutimiza jambo, lengo, gharadhi. Wahenga waliosema "Penye nia pana njia" walikuwa na maana kuwa ikiwa mtu ana dhamira ya kufanya jambo hawezi kukosa njia.

Hii ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kwamba tuwapo na nia ya kufanya jambo fulani lazima tufanikiwe.

"Hakuna kubwa lisilo ukomo." Kwamba kila jambo lina mwisho wake. Hata maisha ya mwanadamu hufikia kikomo chake. Methali hii hutumiwa kumliwaza mtu anayepambana na hali ngumu au matatizo kuwa anapaswa ajitahidi kuvumilia kwani hatimaye yatafikia kikomo chake.

Aidha, "Hakuna kubwa lisiloshindwa." Maana yake hakuna jambo lisilowezekana. Methali hii hutumiwa kumhimiza mtu anayekabiliana na hali ngumu kuwa lazima atafanikiwa hatimaye.Vijana wa 'Bandari ya Salama' (Dar es Salaam) husema: " Kutesa kwa zamu" kwamba ukitesa leo kesho utateswa wewe!

Hapa nazizungumzia timu za Yanga na Simba zenye wanachama na mashabiki (watu wenye mapenzi na hamasa kubwa kuhusu timu zao) wengi nchini na nje ya Tanzania.

Ushahidi ni kwamba timu za Yanga na Simba zinapokwenda mikoani kupambana na timu za huko hupata washangiliaji wengi zaidi kuliko timu wanazopambana nazo mikoani!

Ni ajabu lakini ndio ukweli ulivyo na hii husababishwa na chuki kati ya Yanga na Simba waliokuwa pamoja kabla ya kutengana na kuwa maadui ingawa eti wanaitwa watani wa jadi!

Kwa nielewavyo, 'utani' ni taratibu au desturi za kimila ambazo huwafanya watu wanaojuana waweze kuambiana au kutendeana jambo lolote la mzaha bila ya kuleta chuki au kero; maneno ya masihara; dhihaka.

Utani wa Yanga na Simba ni zaidi ya masihara kwani utani wao umeegemea zaidi kwenye chuki dhidi ya maendeleo ya upande mwingine. Huo sio utani bali ni chuki na kuoneana gere.

Bila kubwabwaja, yaani kusema maneno mengi yasiyoafikiana na lengo langu, nathubutu kusema timu ya Simba, maarufu kwa jina la 'Wekundu wa Msimbazi' wana nafasi nzuri ya kutwaa sio ubingwa wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara tu, bali pia hata ule wa Bara la Afrika, kwa mara ya kwanza kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na baadhi ya nchi jirani yaani Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda n.k.

**Tukubaliane kuwa Simba ya sasa si ile ya zamani iliyoipa Yanga nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara nyingi zaidi hata kuitwa 'mabingwa wa kihistoria.' Hii ni Simba iliyo tofauti kabisa inayoendeshwa na bilionea kijana aitwaye MO Dewji.**

Nakubaliana na wahenga waliosema. "Hakuna kubwa lisilo ukomo." Kwamba kila jambo lina mwisho wake.

"Kweli ndio fimbo ya kukamata" chambilecho wahenga, kwamba kweli ni silaha nzuri maishani. Methali hii yatukumbusha umuhimu wa kuusema ukweli hata kama kwa kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Tukubaliane kuwa Simba ya sasa si ile ya zamani iliyoipa Yanga nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu mara nyingi zaidi hata kuitwa 'mabingwa wa kihistoria.' Hii ni Simba iliyo tofauti kabisa inayoendeshwa na bilionea kijana aitwaye MO Dewji. Kwa upande mwingine tajiri Yusuph Manji aliifadhili Yanga kwa hali na mali lakini alipoondoka, Yanga ikawa kama yatima yaani mtoto aliyefiwa na mzazi wake!

Sasa klabu hiyo inaendeshwa na kampuni ya GSM inayofanya kila jambo yenyewe kama fedha za usajili wa wachezaji, walimu na benchi zima la ufundi pamoja na mishahara yao, vifaa vyote vya michezo n.k.

Najaribu kufikiria kama sio GSM leo Yanga ingekuwa hali gani? Allahu ya aalam (Mungu ndiye mwenye kujua zaidi.) Kama makanisa na misikiti huendeshwa kwa sadaka za waumini wao kwa nini wanachama na mashabiki wa Yanga na vilabu vingine wasiwe na utaratibu wa kuzichangia ili kuziondoa kwenye ukata (ufukara; umaskini; uhitaji)?

Timu zetu zitaendelea kutegemea matajiri mpaka lini? Vinginevyo ziuzwe kwa matajiri na wanachama wabaki kuwa mashabiki tu.

*marobarnabas@yahoo.com*
*0784 334 096*

# MKUTANO MKUU MAALUM WA CCM




Wajumbe wakiwa na mabango yanayoonyesha mikoa waliyotoka wakishangilia burudani iliyokuwa ikitolewa katika mkutano huo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais, Samia Suluhu Hassan, akiwa katika picha ya pamoja na Marais wastaafu, Mzee Ali Hassan Mwinyi na Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo, katika Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, jijini Dodoma jana. **PICHA ZOTE: IKULU**



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda na Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, wakiteta nje ya ukumbi wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM, jijini Dodoma jana. **PICHA: AUGUSTA NJOJI**



ais, Samia Suluhu Hassan, akiwa ameshikilia Tuzo ya Heshima na Pongezi aliyopewa na Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), baada ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti Mpya wa chama hicho.



Viongozi mbalimbali pamoja na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM, wakifurahia wakati wa mkutano huo.

# Kiwanda kikubwa dawa kuanza rasmi uzalishaji

**Na Joseph Mwendapole**

KIWANDA kikubwa cha kutengeneza dawa za binadamu cha Kairuki Pharmaceticals Industries Limited (KPIL) kinatarajia kuanza uzalishaji mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Kairuki, Dk. Muganyizi Kairuki, alisema maandalizi yote yamekamilika na kinachosubiriwa ni umeme na maji.

Dk. Kairuki alisema hata malighafi za kutengeneza dawa zimeshaagizwa kutoka nje ya nchi na zinatarajiwa kufika wakati wowote kuanzia sasa na kwamba wafanyakazi wa kiwanda hicho wameshapatikana.

Pia alisema uwekezaji huo ulioko katika eneo la viwanda Zegeleni, Manispaa ya Kibaha, ni Sh. bilioni 45 ambazo ni mkopo.

Alisema asilimia 60 ya dawa zitakazokuwa zinatengenezwa zitakuwa zikiuzwa kwenye soko la ndani wakati asilimia 40 zitauzwa kwenye soko la nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Kiwanda hicho, alisema kitakuwa na uwezo wa kuzalisha chupa za dawa milioni 55 kwa mwaka na kutengeneza ajira za moja kwa moja 200 na za muda 500.

Alisema watazalisha dawa za aina mbalimbali kwa kutumia teknolojia ya kisasa zaidi, hivyo kupunguza utegemezi wa kununua dawa hizo nchi za nje hivyo kuokoa fedha nyingi.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, juzi alitembelea kiwanda hicho na kusifu uwekezaji uliofanywa na Kairuki na kuahidi kuwa serikali itaendelea kuwawekea mazingira mazuri.

Majaliwa alisema watumishi wa serikali wanapaswa kuwa karibu na wawekezaji hao kusikiliza mahitaji yao kwa wakati badala ya kuwa wasumbufu na kuendekeza urasimu.

Alisema ujenzi wa viwanda vipya kama hivyo ni muhimu kwa kuwa vinaiongezea serikali wigo wa ukusanyaji wa kodi na kutoa ajira kwa vijana wengi. Alisema serikali pekee haina uwezo wa kuajiri vijana wote wasio na ajira.

Alisema serikali itaendelea kulinda viwanda vya ndani kwa kuhakikisha inadhibiti bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kuziongezea tozo ili hata zikiingia nchini zisisambaratishe bidhaa za ndani.



Meneja Mauzo Rejareja wa Puma Energy Tanzania, Venessy Chilambo (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa uzinduzi wa vituo vipya vya mauzo ya mafuta rejareja katika maeneo ya Bukoba, Kihonda Morogoro, Kigamboni, Kijichi, Segera na Tanga. **PICHA: JOHN BADI**

## NMB yapata matokeo mazuri robo ya kwanza

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imesema imeendeleza ufanisi wake kiutendaji katika robo ya kwanza ya mwaka 2021.

Imesema faida ya benki kabla ya kodi imeongezeka kwa asilimia 34 na kufikia Sh. bilioni 93 wakati faida baada ya kodi imeongezeka kwa asilimia 33 na kufika Sh. bilioni 65 katika robo iliyoishia Machi 31 mwaka 2021.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema juzi kuwa ufanisi huo umetokana na ongezeko la mapato, udhibiti wa gharama za uendeshaji na umakini katika utoaji wa mikopo.

Mapato yaliongezeka kwa ailimia 16 na kufikia Sh. bilioni 224 ikilinganishwa na Sh. bilioni 193 za robo ya kwanza mwaka 2020, na mwamba mapato hayo yalichangiwa na ongezeko la pato halisi la riba lililotokana na faida ya mikopo na ile ya kwenye amana za serikali.

Vilevile, mapato yasiyotokana na riba yaliongezeka kwa asilimia 10 kutokana na ongezeko uimarishaji wa utoaji suluhishi za kibenki kwa njia ya kidijitali.

Alisema benki bado ina ufanisi wa kutosha. Utekelezaji wa mikakati ya kupunguza gharama za uendeshaji unaendelea kutoa matokeo chanya kwani uwiano wetu wa gharama na mapato umeimarika mpaka asilimia 48 katika robo ya kwanza mwaka 2021 kutoka asilimia 52 katika robo ya kwanza mwaka 2020, chini ya kiwango kilichowekwa na msimamizi wa mabenki yaani Benki Kuu ya Tanzania (BOT) cha asilimia 55.

Kwa mujibu wa Zaipuna, benki itaendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza gharama na kuongeza ufanisi kwa mujibu wa malengo makuu ya kimkakati ya benki, huku tukiendelea kuwahudumia vyema wateja wake.

Akizungumzia ufanisi na uimara wa benki, Zaipuna alisema: "Tumeanza vizuri. Tunahakikisha ongezeko la thamani kwa wanahisa wetu na nchi kwa ujumla. Matokeo haya ya Q1 yanaakisi uwezo wa kuendelea vyema huko mbele katika utekelezaji wa mikakati yetu kwa kutumia wafanyakazi wetu wanaojitoa kuhudumia wateja wetu kwa ufanisi mkubwa."

# Kampuni za kigeni zamiminika TIC kusaka fursa uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO Cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimeleta kampuni nyingi kwa ajili ya kuwekeza nchini kwa kuwatumia mabalozi wa Tanzania nje ya nchi na wale wanaoziwakilisha nchi zao nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, alisema jana kuwa mwaka jana pekee kwa kushirikiana na ofisi za ubalozi, ilipokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kutoka Korea, Marekani, India, Uturuki, Austria, Japan na Poland.

Alisema kampuni zilizokuja kutafuta fursa zilikuwa 87 ambazo kutoka Ulaya zilikuwa saba, Asia sita, Afrika sita, Amerika mbili na Austria.

Dk. Kazi alisema TIC imeshiriki makongamano 12 ya uwekezaji kwa njia ya mtandao yakiwamo manne ya kilimo, utalii, pamba na korosho yalikuwa ya kisekta wakati makongamano manane ya uwekezaji kwa nchi husika au kanda yakiwa kwa nchi za India, Philippines, Indonesia, Thailand, Afrika Kusini, Quatar, China na Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Alisema kampuni za kigeni zilizokuja rasmi mwishoni mwa mwaka jana kutafuta fursa za uwekezaji zilitoka India, Marekani, China, Falme za Kiarabu, Afrika Kusini na Sweden.

Alizitaja nchi zingine kuwa ni Yemen, Kenya, Ujerumani, Urusi, Australia, Botswana, Misri, Ufaransa, Korea, Austria, Poland, Srilanka, Canada na Ukraine.

Kwa mujibu wa Dk. Kazi, katika siku za karibuni wawekezaji wengi na mabalozi na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa wameonyesha kufurahishwa na mwenendo wa serikali katika suala zima la kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Pia alisema tayari mabalozi na wawekezaji hao wameonyesha nia ya kusaidia program mbalimbali za maboresho ya mazingira ya uwekezaji nchini .

Dk. Kazi alisema TIC itaendelea kuibua fursa a uwekezaji katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR na kitafanya utafiti ili kutoa fursa kwa wawekeaji kubaini maeneo yanayofaa kuwekezwa na kuwezesha reli ya SGR kufanyakazi kwa ufanisi.

Alisema kituo kitaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa mwaka huu wa fedha wamefanya makongamano manne mikoa ya Mbeya, Singida, Katavi na Pwani.

Dk. Kazi alisema kampuni za wawekezaji wa Kitanzania zilizofika kituoni rasmi kwa ajili ya kufuatilia fursa ni 77 kwa kipindi cha Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu.

Alisema kituo katika kuendelea kunadi miradi ya uwekezaji tayari imeandaa miradi 81 ambapo miradi 11 ya watu binafsi pia imepokelewa na kuwekewa utaratibu wa kuinadi kwaajili ya kupata ubia.

Kuhusu usajili wa miradi ya uwekezaji, Dk. Kazi alisema TIC imefanikiwa kusajili miradi 151 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 987, kuanzia Julai mwaka jana hadi Machi mwaka huu iliyozalisha ajira 13,857.

Alisema katika kipindi cha Januari mwaka huu hadi Mwezi Machi TIC imefanikiwa kusajili miradi 51 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 451 iliyochangia ajira 4,272.

Hata hivyo, alisema janga la Corona lilisababisha uwekezaji kote duniani kusuasua na kwamba kusingekuwa na ugonjwa huo usajili wa miradi ungekuwa umefikia hakua kubwa sana.



## HABARI DODOMA

# Wadau wachambua bajeti Madini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MTANDAO wa HakiRasilimali umefanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Madini na kutoa mapendekezo mbalimbali ikiwamo kuboresha sheria na kanuni ili Bunge litimize wajibu wake wa kuhakikisha mapato ya nchi hayapotei.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Rachel Chagonja, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akieleza uchambuzi wa makadirio hayo kwa mwaka 2020/21 na 2021/22 uliofanywa na mtandao huo.

Alisema uboreshaji huo utasaidia Bunge kupokea na kujadili ripoti za Taasisi ya Uziduaji katika Sekta za Madini na Nishati (TEITI).

Chagonjwa alisema pamoja na nia njema ya wizara katika kuongeza uwezo wa taasisi zake kama TEITI kwa ajili ya kuongeza uwazi na uwajibikaji, imeonekana wazi kwamba kuna ukosefu wa utashi wa kisiasa kwenye kutoa fedha kwa ajili ya TEITI.

"Taarifa ya TEITI za miaka 10 (2009 hadi 2019) juu ya mlinganisho wa malipo yaliyofanywa na kampuni za madini kwenda serikali ya Tanzania na kulinganisha risiti za malipo hayo zimeonyesha Sh. Bilioni 90 na dola za marekani 328,000 zimekosa maelezo kuonesha zilipo,"alisema.

Alisema pamoja na kufanyika ukaguzi maalum na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), taarifa za ukaguzi hazijawekwa wazi kwa ajili ya kujadiliwa na wadau kama ilivyo kwa taarifa za kawaida za TEITI.

"Kwa sababu ya namna ya mikataba ya madini ilivyotiwa saini, wajibu wa CAG kwenye sekta ya uziduaji unakuwa kama mtazamaji na kumnyima fursa ya kufanya ukaguzi wa miradi hiyo. Ni katika mazingira maalum tu ndipo TEITI inaweza kumwita CAG kwa ajili ya kufanya ukaguzi," alisema.

"Kwa ujumla kunyimwa huku kwa CAG kukagua mikataba hiyo ni kinyume na Katiba ya Tanzania Ibara ya 143 kuhusu kupata taarifa kifungu cha 5 na 15 cha Sheria ya Ukaguzi ya mwaka 2008," aliongeza.

Alishauri wizara ielekeze rasilimali fedha kwa taasisi ya TEITI ili kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kupunguza vitendo vya kifisadi katika sekta hiyo.

Pamoja na hayo, mkurugenzi huyo alitaja mapendekezo mengine kuwa ni uwapo wa chanzo cha kimkakati cha mapato ili kusaidia kwa uhakika utekelezwaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyopangwa.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya HakiRasilimali, Flaviana Charles, alisema pendekezo lingine ni kuhakikisha wawekezaji katika uchimbaji madini wanatoa fedha na kuingiza mfuko wa mazingira ili wanapomaliza uchimbaji mazingira yarudishwe kwenye hali ya kawaida.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi (kulia), akishiriki futari na wananchi wa Mji wa Chamwino Ikulu, mkoani Dodoma juzi jioni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kasi maambukizi VVU kwa vijana yatisha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amesema hali ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU), kwa kundi la vijana yapo juu huku utafiti ukionesha kati ya watu 72,000 wanaopata maambukizi mapya kwa mwaka asilimia 40 ni vijana.

Katambi alisema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka wa wadau unaotekeleza afua za VVU na UKIMWI zinazowalenga wasichana balehe na wanawake vijana.

Alisema utafiti huo ulifanywa mwaka 2016/17 na kwamba kati ya idadi hiyo ya vijana, asilimia 80 ni wasichana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 na kuwataka vijana kuendelea kuchukua tahadhari ili kujikinga na maambukizi hayo.

"Hii inamaanisha kuwa kila kundi la vijana 10 wenye maambukizi wanane kati yao ni vijana wa kike na wawili ni wa kiume, hivyo ni muhimu kuhimiza vijana na watu wote kupima ili kujua hali zetu, kutumia dawa kama tutagundulika tunaishi na VVU na kuepuka maambukizi ikiwa bado hatujapata maambukizi," alisema.

Alisisitiza UKIMWI bado upo nchini licha ya kuwa na mwelekeo mzuri wa kushuka kwa maambukizi. Alisema hali si nzuri hasa kwa vijana.

Naibu Waziri alisema kuna juhudi zinazofanywa kupitia miradi ya DREAMS Initiatives, Ujana Salama, na Timiza Malengo ambayo inalenga kuwafikia mabinti balehe na wanawake vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 walio kwenye mazingira hatarishi, wakiwamo waliozaa kwenye umri mdogo.

Alisema mradi wa DREAMS unatekelezwa katika mikoa minne na halmashauri 12 na kwamba mradi wa Ujana Salama unatekelezwa katika mikoa minne na halmashauri 11 huku mradi wa Timiza Malengo ukitekelezwa katika mikoa mitano na halmashauri 18.

Alitoa wito kwa mabinti waliojiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali kuwa mabalozi na walimu kwa wasichana balehe na wanawake vijana.

Naibu Waziri Katambi alisema serikali itaendelea kuhakikisha inatoa fedha kwa ajili ya vijana huku akiwataka kuchangamkia fursa za mikopo zinazotolewa katika halmashauri nchini.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, alisema lengo la kikao hicho ni kuwaleta wadau na kuona wamefikia wapi na wamekutana na kero zipi ili kuzitatua.

"Tulianzisha Kijiji Maalum kwa vijana ambayo inalenga masuala ya vijana na haya yote yalikuwa maagizo ya Waziri Mkuu na ni kutokana na kundi hilo kuwa hatarini, na kuongoza kwa maambukizi mapya," alisema.

Balozi Mwakilishi wa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana, Rosemary Shani, alisema wanakabiliwa na upungufu wa vituo vya kutolea huduma kwa vijana, soko la uhakika wa bidhaa wanazozalisha na uelewa mdogo wa jamii kuhusu kinga za VVU.

# Utendaji TADB wamkuna Waziri

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema utendaji mahiri wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), umesaidia kuleta mageuzi kwenye sekta za kilimo, uvuvi na ufugaji nchini.

Akipokea taarifa ya utendaji wa kimkakati wa TADB iliyowasilishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Japhet Justine, ofisini mwake jijini hapa, alisema utendaji mahiri wa TADB unasaidia kuyapa nguvu maono ya Rais Samia Hassan juu ya kilimo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alieleza kuridhishwa na ripoti ya benki hiyo na kusema anaona jitihada ya dhahiri ya benki hiyo katika kuendeleza na kutimiza wajibu uliowekwa na serikali ili utimizwe na taasisi hiyo.

Awali, Justine alisema tangu kuanzishwa kwa benki hiyo zaidi ya wakulima 1,800,000 wamefikiwa.

"Kipekee Waziri tumeshawishi kushuka kwa kiwango cha riba zilizokuwa zikitolewa na benki na taasisi za kibiashara za fedha kutoka asilimia 24 hadi kuwa kati ya asilimia 17 na 14," alisema.

Alibainisha kwamba malengo mengine ya benki hiyo ni kufungamanisha wakulima wanaozalisha mazao na masoko na kuboresha miundombinu ya kilimo kwa kuhakikisha upatikanaji wa zana bora za kilimo na uvuvi, upatikanaji wa pembejeo na viwatilifu kwa wakulima.

**Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alieleza kuridhishwa na ripoti ya benki hiyo na kusema anaona jitihada ya dhahiri ya benki hiyo katika kuendeleza na kutimiza wajibu uliowekwa na serikali ili utimizwe na taasisi hiyo.**



# HESLB, bodi mikopo Zanzibar zatia saini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, amesema makubaliano kati ya Bodi ya Mikopo ya Zanzibar pamoja na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania yataziwezesha taasisi hizo kufanya kazi kwa ushirikiano katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi.

Akizungumza jana mjini Zanzibar katika hafla ya utiaji saini ya makubaliano ya ushirikiano kati ya bodi hizo, Katibu Mkuu huyo alisema makubaliano hayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia kupanua huduma za mawasiliano pamoja na vikwazo vya urudishaji wa mikopo.

Alisema taasisi hizo mbili majukumu yake yanafanana ambayo ni kutoa huduma za mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa mujibu wa sheria ya kuanzishwa kwazo.

Juma alisema kufikiwa kwa makubaliano hayo sasa kutaziwezesha taasisi hizo kufuatilia kwa karibu wanafunzi katika urejeshaji wa mikopo ili itumike kwa wanafunzi wengine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo Zanzibar, Iddi Khamis Haji, alisema bodi inakabiliwa na changamoto kubwa ya urudishaji wa mikopo na kwa sasa fedha nyingi zimetolewa lakini ziko mikononi hazijarudi katika bodi.

Alisema katika kipindi cha miaka kumi Bodi ya mikopo ya elimu ya juu imetoa mikopo ya Sh. bilioni 66 lakini urejeshaji wake ni wastani wa Sh. bilioni tatu kwa mwaka.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-razak Badru, alisema makubaliano hayo yamekuja katika wakati mwafaka ambapo viongozi wa juu wa serikali akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, wamesisitiza ushirikiano na taasisi zenye uhusiano katika Muungano kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Pia alisema makubaliano hayo yatasaidia kuwatambua na kuhakiki wanafunzi wanaopata mikopo kwa upande wa Zanzibar ili wasipate mikopo tena inayotolewa na HESLB.



Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Zanzibar, Omar Said Shaaban (kushoto), akizungumza na Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Frederic Clavier, aliyemtembelea ofisini kwake, Unguja juzi. Walizungumzia masuala mbalimbali ya kibiashara baina ya nchi hizo mbili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkuu mpya JKU akataa utegemezi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAPIGANAJI wa vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wametakiwa kuongeza uzalishaji wa chakula ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa taasisi hizo na kuacha kutegemea mgawo wa serikali.

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), Kanali Makame Abdalla Daima, alisema hayo jana wakati akizungumza na wapiganaji wa kikosi hicho alipokuwa akijitambulisha kutokana na uteuzi wake uliofanywa hivi karibuni na Rais Dk. Hussein Mwinyi.

Alisema malengo ya kikosi hicho ni kuongeza uzalishaji na kujitegemea kwa kutumia rasilimali zilizopo yakiwamo mabonde ya mpunga.

Kanali makame alisema wakati umefika hivi sasa wa kulima kilimo cha miwa ambacho soko lake ni la uhakika katika kiwanda cha kuzalisha sukari cha Mahonda.

"Hatuna sababu ya kushindwa kuzalisha chakula kwa wingi ikiwamo mpunga pamoja na miwa kwa sababu maeneo ya kilimo yapo pamoja na mabonde ya uzalishaji wa mpunga," alisema.

Akimkaribisha mkuu mpya wa JKU baada ya makabidhiano ya ofisi na nyaraka mbalimbali, aliyekuwa mkuu wa jeshi hilo, Ali Mtumweni Hamad, aliutaka uongozi wa mpya kujipanga zaidi na kuyafikia malengo ya kujitosheleza kwa chakula.

Aidha alimtaka mkuu mpya wa kikosi hicho kufuatilia mipaka pamoja na hatimiliki ya majengo ya kambi za kikosi cha (JKU) ili kuepuka uvamizi na migogoro na wananchi.

"Malengo na mikakati ya JKU tangu ilipoanzishwa ni kujitosheleza na chakula kwa kutumia rasilimali ziliopo malengo ambayo bado hayajafikiwa hadi sasa," alisema.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar (Magereza), Luteni Kanali Khamis Bakari Khamis, aliwataka watendaji wa chuo hicho kudumisha nidhamu katika kutoa huduma kwa wafungwa na watuhumiwa wa makosa mbalimbali.

Alisema katika kipindi chake atahakikisha anakiongoza chuo hicho na kuleta mabadiliko makubwa yakiwamo ya kiuchumi na kuwiwezesha vikosi kutumia rasilimali zake kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Khamis alisema matarajio yake makubwa kupata ushirikiano kutoka kwa maofisa pamoja na wapiganaji wote ili kutekeleza malengo hayo.

"Ili nifanikiwe katika utekelezaji wa majukumu yangu, nawaomba wapiganaji pamoja na maofisa wote mnipe ushirikiano ili kufikia malengo ya kuteuliwa kwangu," alisema.

# Othman akemea urasimu serikalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATUMISHI na watendaji wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na taasisi zake, wametakiwa kuongeza ufanisi na kuondoa urasimu ambao ni kikwazo katika uwajibikaji na kuwatumikia wananchi.

Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na wakuu na watendaji wa ofisi yake huko Pemba ikiwa ni ziara ya kujitambulisha kwa wakuu wa taasisi zilizoko chini ya ofisi yake.

Alisema moja ya matatizo makubwa na kero kwa wananchi ni viongozi waliokabidhiwa majukumu kushindwa kufikia malengo ikiwamo urasimu katika kuwatumikia wananchi.

Othman alisema serikali ya Zanzibar imedhamiria kuwatumikia wananchi na kutoa huduma kwa ufanisi na kuondosha urasimu na usumbufu usiokuwa na sababu yoyote.

"Hiyo ndiyo dhamira na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi. Sisi watendaji wake tunawajibika kutekeleza maagizo hayo ya kuleta ufanisi na kupambana na urasimu ambao ni kikwazo katika kuyafikia malengo hayo," alisema.

Kuhusu taasisi zilizo chini ya ofisi yake, aliwataka watendaji kuongeza kasi ya kupambana na matumizi ya dawa za kulevya ambayo yamesababisha athari kubwa kwa jamii ikiwamo vijana ambao ndio nguvu kazi ya taifa.

Pia alikitaka kikosi kazi cha kupambana na uingizaji wa madawa ya kulevya kuimarisha ulinzi katika maeneo makuu ya kuingia watu ikiwamo katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar pamoja na maeneo ya bandari.

Alisema mikakati zaidi inahitajika katika kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya kutokana na mazingira ya kijiografia ya visiwa vya Unguja na Pemba vyenye njia nyingi za kuingia pamoja na bandari zisizo rasmi.

"Watendaji wa kitengo cha kupambana na madawa ya kulevya tunakabiliwa na changamoto nyingi. Tunatakiwa kuongeza ufanisi zaidi katika kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya ikiwamo katika maeneo ya bandari bubu," alisema.

Sambamba na hilo, aliwataka watendaji kutoa elimu zaidi juu ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kufikisha taarifa hizo kwa haraka.

Aliwataka wananchi nao kuchukuwa tahadhari ikiwamo kuacha kufanya uharibifu wa mazingira kwa kuchota mchanga wa pwani kwa matumizi ya shughuli mbali mbali ikiwemo ujenzi.

Naye Matibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Khadija Khamis Rajab, aliwataka watendaji wa ofisi hiyo kufahamu kwamba wanakabiliwa na majukumu makubwa ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja katika maisha yao.

Alisema mapambano dhidi ya ukimwi, udhibiti wa dawa za kulevya pamoja na mikakati ya kuimarisha mazingira kutokana na mabadiliko ya tabia nchi ni moja ya majukumu ya ofisi hiyo kuona malengo yote yanafikiwa kwa mafanikio makubwa.



**PROFESA JAY**

UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII

BT BURUDANI TELE

JUMAMOSI MEI 1, 2021



IDRIS Sultan ameweka rekodi ya kuwa Mtanzania wa kwanza ambaye ataonekana katika uwanja mpana wa mtandao wa filamu duniani Netflix katika tamthilia ya Slay On.

Mara baada ya filamu hiyo kutambulishwa rasmi mastaa na viongozi mbalimbali wamejitokeza kumwagia sifa Idris, kwa kupiga hatua kubwa.

Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete, alitumia muda wake kumwandikia ujumbe kupitia mtandao wa Twitter, akimpongeza na kuelezea furaha yake kuona kijana wa Kitanzania anaonekana kwa mara ya kwanza katika mtandao huo maarufu.

Kikwete ametoa hamasa kwa wasanii wengine kuiga mfano huo ili siku moja Tanzania iwe inasifika katika tasnia ya sanaa.

Akizungumza katika mahojiano na kituo kimoja cha televisheni, Idris ameeleza furaha yake kuona kiongozi mkubwa kama yeye anampongeza kwa kumwandikia ujumbe, kitu ambacho kimempa faraja na kujiamini.

Amesema tamthilia ya Slay On ambayo imejikita katika vichekesho, amecheza katika nafasi ya mhusika mkuu kitu ambacho ni kigumu hasa kwa kuzingatia wasanii walioshiriki wametoka katika mataifa tofauti ya Afrika na Marekani.

"Kupewa nafasi ya uhusika mkuu katika filamu inayowashirikisha mastaa wa uigizaji barani Afrika na Marekani ni jambo gumu na unaweza kusema Mungu ameonyesha uwezo wake kwangu," amesema.

Amesema sasa ameanza kupata njia ya kwenda katika uwanja mkubwa wa Hollywood, kwani kupitia filamu hiyo watayarishaji wakubwa watamuona na kumjumuisha katika kazi zao.

"Siwezi kufikiria kazi hii pekee, natarajia watayarishaji wakubwa wa Hollywood wataniona na pengine kunipa ofa za kushiriki katika filamu zao," ameongeza kusema.

# SLAY

## Filamu inayodatisha Watanzania

## BASI SAWA

### Idris unawajua watoto wa IG?

MCHEKESHAJI na mwigizaji kutoka Bongo, Idris Sultan, ameibua mjadala mkali baada ya kuhoji baadhi ya mastaa ambao wana kawaida ya kuwafungulia watoto wao akaunti za mitandao ya kijamii baada ya benki.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Idris amejiuliza kwa nini mastaa hao mara wanapopata watoto wao kitu chao cha kwanza ni kufungua kurasa za mitandao, huku wakitupa mbali akaunti za benki kwa ajili ya kuhifadhi pesa zao.

"Siku hizi tukipata watoto tu cha kwanza ni IG Account, Bank Account atajijua mwenyewe, 'likes' za ndugu zetu zitawasomesha nadhani, hapo tunawapa presha kuwa ni lazima kuiendeleza hiyo kurasa wakikua, itakuaje kama hawataki mitandao ya kijamii wanataka kuwa maspai".



### Brian kweli muungwana

RAPA Brian Simba, amesema kwa sasa hayupo kwenye lebo ya Mdee Music, inayomilikiwa na Vanessa Mdee, baada ya mkataba wake kufikia ukingoni.

Brian amemshukuru Vanessa Mdee kwa kufanya nae kazi ambayo imempa uzoefu mpya kwenye upande wa muziki.

"Masomo hayajanirudisha nyuma yamenipa uzoefu mpya kwenye maisha, kufanya kazi na Vanessa Mdee ilinisaidia vitu vingi kama kuzunguka mikoa na nchi mbalimbali, ilikuwa uzoefu mzuri ila mkataba wetu wa kufanya kazi uliisha" amesema Brian Simba





## Profesa Jay awakumbuka wanakitaa

MWANAMUZIKI mkongwe, Profesa Jay, amewakumbusha mashabiki wake kuwa kurudi kwake jukwaani ni kutaka kuwalipa kile walichokosa wakati akitumikia wananchi wa Mikumi.

Profesa Jay, ametangaza kuwapatia zawadi mashabiki hao kwa kutambulisha Albam yake mpya itakayotoka hivi karibuni.

"Nilikuwa nina deni kubwa kwa mashabiki, nataka niwape furaha waliyokosa kwa muda mrefu, nitakuja na Album mwaka huu, mimi ni Shule pia mwalimu mkuu wa chuo cha kitaa na nitawaletea Album ambayo itakuwa kama kitabu na nyimbo zake zitakuwa kama vifungu

## Tumaini: Bora ujinga, kuliko upumbavu

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE Jamii yetu hasa ya Kiafrika, kuna mila na utamaduni mzuri sana na zinafaa kuigwa na watu wa mabara yote duniani. Afrika ndiko kuna tamaduni za mdogo kumheshimu mkubwa. Watu kuheshimiana. Kuishi kijamaa na kama ndugu. Kuwasaidiana kwenye shida na raha. Lakini kwenye bara hili pia kuna mila mbaya ambazo zinapaswa kukemewa. Ni kama vile mila za kuoa wake wengi. Kukeketa na hata imani za kishirikina kwenye vitu ambavyo ni vya kisayansi tu.

Hili linathibitishwa kwenye filamu ya 'Tumaini' ambayo imebeba dhana nzima ya maisha ya jamii za Kiafrika na hasa zile zinazoishi vijijini ambapo baadhi yao hawana elimu.

Inaanza kuonyesha kijana Gatho anafukuzwa na wanakijiji baada ya kubambwa anaiba kuku. Anakimbilia kwenye nyumba moja hivi. Ni nyumba ya marehemu mzee Mwaka. Alikuwa amefariki miezi michache iliyopita. Kijana wake Gamba alikuwa amekwenda mjini kujenga kaburi la baba yake. Alimficha Gatho na hakuwaambia wanakijiji waliokuwa wanamfukuza. Alipomuuliza kwa nini anaiba hakupewa majibu ya kuridhisha.

Siku chache baadaye anakutana na msichana njiani ambaye anamshukuru kwa kumficha kaka yake.

Kesho yake anafuatwa na baadhi ya wanakijiji, akiambiwa kuwa anaonekana akiwa na Gatho pamoja na dada yake Tumaini, watu ambao wametengwa na kijiji.

Gamba anafanya uchunguzi mdogo na kugundua kitu. Ni kwamba Tumaini na Gatho wanaishi peke yao baada ya wazazi wao kufariki. Lakini wametengwa na wanakijiji. Ila Tumaini, pamoja na kuwa ni msichana mzuri, lakini ana matatizo ya kutokwa na haja ndogo bila kizuizi. Kijiji chote kinaamini ni laana. Na alichogudua ni kwamba walikwenda kwa mganga na kuambiwa ili apone, ni lazima wapatikane kuku watatu na mahindi. Kijiji kiligoma kuwauzia mahindi na kuku. Ndiyo maana Gatho anaiba ili apate vitu vitakavyopelekwa kwa mganga na kutengua laana hiyo, au kurogwa huko.



Gamba akaamua alivalie njuga suala lile. Akajua kabisa wala si laana ila Tumaini anaumwa Fistula.

Ni ugonjwa ambao ulimfanya hata kuachwa na mpenzi wake Longi. Wanawake kijijini wakawa anamcheka na kumsengenya. Gamba akampeleka zahanati kupata matibabu. Tumaini anapona. Longi anamtaka tena Tumaini. Sasa Tumaini hamtaki tena. Anamkata Gamba.





## Miss Bella utawafunga wengi

MSANII wa Muziki wa Bongo Fleva, Miss Bella kutoka kundi la 'Scorpions girl', amesema wasanii ambao wanaendekeza kiki zisizo na maadili wachukuliwe hatua za kisheria.

Miss Bella amesema endapo mtu ataonekana kufanya kiki au vitu visivyo na maadili mitandaoni kusiwe na haja ya kuchelewa, kwani haraka apelekwe mahakamani na akipatikana na hatia afungwe.

"Msanii anafanya tukio leo anapelekwa mahabusu ila kabla ya saa 24 unamkuta nje, kwa hiyo hata wengine wanapata nguvu ya kurudia, sheria ifuate mkondo wake kwa uthibiti zaidi kama mtu anafanya kosa apelekwe mahakamani moja kwa moja afungwe, ningeishauri Serikali kama inatakiwa itoke hukumu itolewe haina haja ya kuchelewa" ameeleza Miss Bella

## WAKONGO WALIOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliangalia 'kolabo' kali ambazo wanamuziki na wasanii kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo walizifanya na wanamuziki na wasanii wa Kitanzania.

Na hii ni baada ya mwanamuziki nguli nchini huko, Awilo Longomba kutoa wimbo akiwa pamoja na msanii wa Tanzania, Harmonize walioiita 'Attitude'.

Tuliangalia 'kolabo' kadhaa, ikiwamo hata ya msanii Diamond Patinumz na Koffi Olomide, iliyopewa jina la 'Waah'.

Leo hatutokwenda mbali sana. Tutaangalia ziara za wanamuziki wa Kikongo au bendi ambazo zilitikisa na kuwapa mhaho mashabiki wa muziki nchini, wanajazana kwenda kutazama shoo zao.

**Franco na TP Ok Jazz**

Tanzania ilipata ugeni mkubwa mwaka 1975 wakati kundi zima la TP OK Jazz chini ya kiongozi wake, Lwambo Luanzo Makiadi Franco lilipotua nchini kwa mwaliko wa chama cha TANU kwenye sherehe za kuzaliwa kwake, kabla haijaitwa CCM.

Kwenye Uwanja wa Taifa, kwa sasa Uhuru ilikuwa balaa. Watu walijazana kupita kiasi na nyimbo nyingi za zamani na mpya kwa wakati huo zilipigwa na kukonga nyoyo za watu wengi wakati huo.

Kikubwa zaidi ni wingi wa vyombo walivyokuja navyo na ilikuwa mara ya kwanza kushuhudia vyombo vya aina ya Ranger nchini ambavyo vilisafirishwa na malori ya CORETCO, kutoka bandari ya Ziwa Tanganyika Kigoma vikitokea Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo hadi Dar es Salaam.

Kutokana na nguvu ya vyombo hivyo, na wakati huo Dar haikuwa na magorofa mengi na bado ilikuwa ndogo inasemekana muziki ulikuwa unasikika laivu Dar nzima. Alifariki mwaka 1989.

**Tabu Ley Rochereau**

Mpinzani mkubwa wa Franco, Tabu Ley, yeye alifanya ziara nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 1980 kwa mwaliko wa chama tawala, lakini sasa wakati huo ikiitwa CCM.

Alikuja na mwanamama Mbilia Bel wakati huo ameshaanza kuwa maarufu. Ilikuwa balaa kubwa kwenye ukumbi wa Diamond Jubilee ambapo bendi ya Afrisa Intenational ilipofanya shughuli yake, nyimbo za 'Nadina', 'Nakei Nairobi' na 'Maze' zikitamba. Alifariki mwaka 2013.

**Pepe Kalle na Empira Bakuba**

Kwa mara ya kwanza, mwanamuziki mwenye umbile kubwa, mrefu futi sita na nchi kadhaa, huku akiwa na miraba minne aliwasili nchini Tanzania mwaka 1989, akifanya ziara Arusha na Dar es Salaam. Wakati huo akitamba na kibao chake cha 'Pon Moun Paka Bouge' na alipoondoka alitoa kibao cha 'Hidaya'. Alirejea tena nchini Tanzania katikati ya miaka ya 1990 wakati huo akitamba na ngoma kama 'Roger Milla' na alipoondoka alitoa wimbo wa 'Yanga Afrika'. Alifariki mwaka 1998.

**Kanda Bongoman**

Ndiye mwanamuziki aliyekuja Tanzania na kupiga kwa kiingilio kikubwa zaidi. Ilikuwa ni mwanzoni mwa miaka ya 1990. Kiingilio kilikuwa ni Sh. laki moja. Watu walijaa Kilimanjaro Hotel na wengine kushindwa kuingia wakiwa na tiketi zao mkononi. Kandabongoman aliwateka Wabongo kwa nyimbo za 'Isambe', 'Moni', 'Muchana', Wallow','Bili', 'Liza', 'Kadhi' na nyingine nyingi.



**JB Mpiana na Wenge Musica**

Ilikuwa ni katikati ya miaka ya 1990, bendi iliyoondokea kupendwa na vijana wa wakati huo ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Wenge Musica ilipofanya ziara nchini Tanzania ikiwa na mwimbaji wake tegemeo, JB Mpiana, kiwamo Werrason na wengineo, wakifanya mambo makubwa na kuleta mabadiliko hata kwenye muziki wa Tanzania, bendi za Diamond Sound, Twanga Pepeta, FM Academia zikaanzishwa.

# Khloe kumbe alivumilia mengi

NYOTA wa mpira wa kikapu Marekani, Tristan Thompson, ameshutumiwa kujihusisha kimapenzi na wanawake wengi, wakati akiwa katika ndoa ya mama wa mtoto wake, Khloe Kardashian.

Kulingana na mwanamke mmoja anayefahamika Sydney Chase, aliandika katika ukurasa wake wa Instagram kuwa, Tristan hasemi kweli katika suala la wanawake wa nje pale anapokutana na Khloe, ambaye ni mshiriki wa kipindi cha maisha cha familia ya Kardashian.

Amesema hata yeye alipokutana na mwanaume huyo alimwambia hana mke, hivyo alikuwa akijirusha akiamini hivyo mpaka alipokuja kupata ukweli.







## Rapa Nigeria apata ajali mbaya

Rapa na mwimbaji kutoka Nigeria, Victony, yupo katika hali mbaya baada ya kujeruhiwa vibaya katika ajali ya gari.

Msanii huyo alipata ajali hiyo April 25, mwaka huu, wakati akitoka katika sherehe ya kuzaliwa ya mwanamuziki nyota Oxlade akiwa na rafiki zake.

Meneja wake, anayeitwa Dafe, kupitia ukurasa wa Twitter, alitoa taarifa akisema Victony amepata majeraha mengi mwilini na sasa amelazwa hospitali moja akipatiwa matibabu.

## Mr P kumbe naye anabet

MWANAMUZIKI aliyeunda kundi la P-Square, Peter Okoye, maarufu kama Mr P, baada ya miaka ya nyuma utabiri wake kwamba timu za Uingereza zingeingia fainali zote mbili za Ulaya kuwa kweli sasa amekuja na utabiri mwingine kama huo.

Utabiri huo ulitimia baada ya ligi ya mabingwa Ulaya kuwakutanisha Liverpool na ile fainali kuchezwa kati ya Chelsea na Arsenal, zote za Uingereza.

Baada ya kufanikiwa katika utabiri huo wa mwanzo, Mr P, amesema sasa msanii huyo ametabiri tena kuhusu fainali za mwaka huu za michuano hiyo ambapo amesema timu zote za Uingereza zitacheza tena fainali.

"Ninachoona tena ni fainali nyingine za Klabu za Kiingereza, nilitabiri hii miaka miwili iliyopita na ikatokea hivyo" ameandika Mr P.

Timu nne zipo katika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo ambapo Chelsea na Manchester City wapo UEFA, halafu Arsenal na Manchester United wapo nusu fainali ya Europa.





## Video ya Baba Ijesha aibu tupu

VIDEO ya mwigizaji kutoka Nollywood, Baba Ijesha, ambayo inamwonyesha akikiri kumnyanyasa binti wa mchekeshaji Princess, imetolewa.

Video hiyo ambayo imekuwa ikienea kwenye mitandao ya kijamii inamwonyesha mwigizaji huyo ambaye anazidi kushutumiwa nchini humo, akiomba radhi na kukiri kufanya kitendo hicho cha aibu.

Pia katika video hiyo inasikika sauti ya Princess, ikielezea kusikitishwa kwake na mwigizaji huyo.

**MAKALA**

# Uagizaji wa pamoja, uwekaji vinasaba ulivyoleta nafuu kwa watumiaji mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

MAISHA ni mafuta na mafuta ni maisha. Usemo huo unaonyesha umuhimu wa nishati ya mafuta kwa maisha ya kila siku ya binadamu. Hiyo inatokana na ukweli kwamba shughuli nyingi za kila siku za kibinadamu zinategemea kwa kiasi kikubwa nishati hiyo.

Hakuna sekta isiyotegemea nishati ya mafuta kwa maana ya petroli na dizeli katika uendeshaji wa shughuli zake za kila siku. Ni dhahiri kwamba bila kuwapo kwa vitu hivyo, maisha ya mwanadamu yanaweza kuwa katika matatizo makubwa.

Mfano ni mwishoni mwa miaka ya 2000 wafanyabiashara walipogoma kuuza mafuta kutokana na kushuka kwa bei wakisingizia kuwa kama wangeuza kwa bei mpya, wangepata hasara. Ulikuwa mtafutano wa aina yake hasa katika jiji la

Dar Salaam kwa kuwa mafuta yalikuwa yakiuzwa katika vituo vichache, hatua ambayo ilisababisha msongamano katika sehemu zilizokuwa zikitoa huduma hiyo.



Mhandisi Godfrey Chibulunje.

Migomo hiyo ya wafanyabiashara ilitokana na kutokuwapo kwa udhibiti wa kutosha wa uingizaji wa mafuta na uuzaji pamoja na upangaji wa bei. Kila kampuni au wauzaji wa rejereja walikuwa wakipanga bei kulingana na hali ya soko ilivyokuwa ikienda jambo ambalo lilisababisha bei kutofautiana ndani ya mji au mkoa mmoja.

Hatua hiyo ya wafanyabiashara kuuza kwa bei wanazotaka ilisababisha bei za mafuta kupanda holela hata mara tatu kwa siku. Wakati mwingine wafanyabiashara hao walikuwa wakikaa na kupanga bei, jambo ambalo lilikuwa kinyume cha kanuni na sheria za ushindani.

**UAMUZI MGUMU**

Yote hayo yalisababisha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na maji (EWURA) kuchukua hatua madhubuti zilizowafanya watumiaji kupata unafuu mkubwa juu ya bidhaa hizo kwa upande mmoja na wafanyabiashara kubanwa, kwa upande mwingine.

Kwa kuanza udhibiti wa bei za mafuta mwaka 2009, bei za Dar es Salaam, mathalan, zilishuka kutoka Sh. 2,000 kwa lita hadi Sh. 1,233 ni punguzo la asilimia 62, kwa mujibu wa EWURA. Aidha, kwa mikoa ya mbali kama Kigoma, bei ilishuka kutoka takribani Sh. 2,400 hadi Sh. 1,642 kwa lita ikiwa ni punguzo la asilimia 52.

Kabla ya hapo bei za mafuta zilikuwa zaidi ya Sh. 2500 kwa lita katika Mkoa wa Dar es Salaam, hali iliyowafanya watumiaji wa bidhaa hiyo kuwa katika wakati mgumu. Hiyo pia ilipandisha hata gharama za maisha.

Katika kufanya hivyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, pia anasema mamlaka hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati iliandaa Mfumo wa Uagizaji wa Pamoja (BPS) wa mafuta.

Mfumo huo, kwa mujibu wa Chibulunje, umesaidia mambo mengi ikiwamo kupungua kwa gharama mbalimbali katika sekta ndogo ya mafuta.

"Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wa Aprili 2014, ulibaini kuwa, kwa ujumla, BPS imesaidia kupunguza gharama jumla ya Sh. bilioni 121.57 kwa mwaka," anabainisha.

Kwa mujibu wa Mhandisi Chibulunje, faida zilizotokana na BPS ni pamoja na kupungua kwa gharama za usafirishaji (premium) kwa Sh. bilioni 81.9 kwa mwaka; kupungua kwa gharama za uhifadhi kwa Sh. bilioni 25.72 na gharama za uagizaji mafuta kwa Sh. bilioni 13.95 kwa mwaka.

"Faida zingine za uagizaji wa mafuta kwa pamoja ni pamoja na kupatikana kwa taarifa sahihi za kiwango cha mafuta kinachoingizwa nchini, hivyo kuongeza mapato ya kodi ya serikali kwa kiwango cha asilimia 24 kwa mwaka 2012," anasema.

Faida zingine, anasema, ni kuongeza ufanisi katika udhibiti wa bei za mafuta kwa kuwa na gharama halisi za mafuta yanayoingia nchini na kurahisisha udhibiti wa ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini.

Kutokana na faida hizo, Chibulunje anasema EWURA itahakikisha BPS inaendelea kutekelezwa kwa ufanisi na itaendelea kuisimamia Wakala wa Uagizaji Mafuta Pamoja (PBPA) na mfumo kwa ujumla. Anasema hiyo ni kutokana na EWURA kuwa na utaalamu mpana zaidi na taarifa za mwenendo wa soko la mafuta ndani na nje ya nchi.

**MANUFAA ZAIDI**

Jambo lolote linapokuwa na mafanikio, hutoa mwanga na wengine kujifunza ili kuleta tija katika nafasi zao. Kuwapo kwa BPS katika mafuta kumesababisha taasisi nyingi nchini kujifunza na kufuata mfumo huo.

Chibulunje anasema taasisi zinazosimamia sekta za afya na kilimo hususan dawa na mbolea zimejifunza juu ya utekelezaji huo. Taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) na Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

**UCHAKACHUAJI KWISHA**

Kabla ya kuanza mfomo wa uagizaji pamoja wa mafuta, kulikuwa na uchakachuaji wa hali ya juu wa mafuta ambao ulikuwa ukisababisha madhara kwa watumiaji na wakati huo huo, serikali kukosa mapato stahiki.

Hali hiyo pia ilitokana na udanganyifu uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wafanyabiashara. Hatua hiyo ilisababisha mamlaka kuanza kupambana na tatizo hilo na hatimaye kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu, EWURA ilichukua hatua kupambana na uchakachuaji, hivyo kuleta mafanikio chanya kwa kupunguza tatizo kutoka asilimia 80 mwaka 2007 hadi asilimia nne mwaka 2020;

"EWURA pia ilianzisha programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi, uchakachuaji na kuweka mazingira ya ushindani wa haki," anasema.

Kutokana na hatua hiyo, utafiti wa UDSM kuhusu matumizi ya vinasaba kwa mwaka 2010 hadi 2013 ulibaini ongezeko la mapato ya serikali kwa Sh. bilioni 468.5. mapato hayo yalitokana na kodi ambazo ni Sh. bilioni 146.5 (mwaka 2010/11), Sh. bilioni 129.8 (mwaka 2011/12) na Sh. bilioni 192.2 kwa mwaka 2012/13.

Sambamba na serikali kupata mapato stahiki kutokana na kodi, uwekaji vinasaba kwenye mafuta kumehakikisha usalama na afya za watu pamoja na mali zao kwa kuwa hakuna athari za kimazingira zinazoweza kutokea wakati wa uendeshaji wa biashara hiyo.

Kanuni za uwekaji vinasaba kwenye mafuta za mwaka 2010 inahusu mafuta yote yanayotumika nchini, isipokuwa yale yaliyosamehewa ushuru na serikali. Kanuni hizo pia zimeainisha adhabu mbalimbali kwa mtu anayekutwa na mafuta yasiyokidhi viwango vya vinasaba.

**MKAZO WA WAZIRI**

Katika kuhakikisha uwekaji vinasaba unasimamiwa ipasavyo, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kuanzia kwenye matanki yanayohifadhi mafuta badala ya magari.

Agizo hilo alilitoa wiki hii alipotembelea maghala ya mafuta ya kampuni za Camel Oil na Oil Com, Kurasini, Dar es Salaam na kukuta wataalam kutoka TBS wakifanya kazi ya uwekaji wa vinasaba kwenye magari ya kusafirisha mafuta.

"Nataka muanze kupima mafuta kuanzia kwenye matangi yenyewe hadi kwenye vituo badala ya kusubiri pale wanapopakia kwenye magari, Je,ikitokea wamepakia wakati hampo, mtajuaje kuwa mafuta husika yana ubora?" alihoji.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha mafuta yanakuwa na ubora, kodi zinapatikana," alisisItiza huku akiagiza EWURA kuhakikisha inasimamia kikamilifu uwekaji wa vinasaba kwenye mafuta.



Waziri wa Nishati, Medard Kalemani (katikati mwenye shati jeupe), akikagua upimaji waq vinasaba katika mafuta. **PICHA:MTANDAO.**

# Awamu ya sita iipe Mei Mosi mwelekeo mwingine

**Na Gaudensia Mngumi**




Vilio vya ujira kiduchu, pensheni ndogo na utumishi usio na tija visiwe maudhui kila mara siku ya Mei Mosi.**PICHA: MTANDAO.**

LEO ni Siku ya Mei Mosi, ambayo wafanyakazi wengi wa Tanzania siku za nyuma waliamini kuwa ulikuwa wakati wa kusikia mambo mazuri kutoka kwa wakuu wa nchi.

Ni siku taifa lilipowasikiliza viongozi wakuu wakiahidi mambo mema kwa wafanyakazi kutokana na ukweli kuwa mwajiri mkuu ni sekta ya umma au serikali kuu na za mitaa.

Kwa miaka mingi ilikuwa siku ya kusikia ahadi za nyongeza ya mishahara na kupanda vyeo hasa ya kwanza hadi ya tano, lakini kwa miaka mitano sasa ilikuwa kama inapoteza muelekeo huo, kwa sababu serikali haikuwa tayari kuongeza mishahara wala maslahi kwa watumishi.

Enzi hizo, Mei Mosi ulikuwa wakati wa maandamano yanayofanyika katika mikoa mbalimbali nchini na pengine kwingineko duniani.

Kwa Tanzania maandamano yaliambatana na sare kila kikundi kikivalia kitenge na kubeba mabango wakijitangaza. Kwa mfano kuna sekretariati ya Shirikisho Huru la Vyama vya Wafanyakazi- TUCTA. Si hao tu na nyuso za bashasha zilionekana pia kwa wanachama wa (RAAWU) Chama cha Watafiti na Wafanyakazi wa Taasisi za Huduma na Elimu ya Juu.

Kuna waalimu- CWT, wapo wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Mahotelini na Majumbani (CHODAWU) na pia wanachama wa TUICO wanaotumika kwenye viwanda na biashara na wanachama wa Wafanyakazi wa Migodi, ndiyo wana-TAMICO.

Kadhalika lipo kundi kubwa la wanachama wa TALGWU ambalo ni jumuiko la wafanyakazi wa Serikali za Mitaa na TUGHE ambacho ni Chama cha wafanyakazi wa Serikali Kuu na Sekta ya Afya.

Mei Mosi mara nyingi pamoja na vitenge na mabango watumishi wanaisherehekea siku yao wakidai na kuomba maslahi bora zaidi na kwa miaka mingi kushinikiza kuwapo na nyongeza ya mishahara ya kima cha chini.

Ujumbe mwingine ni kutaka kupunguziwa kodi ya mishahara (PAYE ) na kukumbusha kuwa licha ya watu kuwa na ajira idadi ya wafanyakazi maskini inaongezeka.

Japo hakuna takwimu za moja kwa moja kuzungumzia hilo, ni ukweli kuwa idadi ya watu wenye ajira inaonekana kama ni kubwa, lakini hata hivyo umaskini unaongezeka kila mwaka kutokana na ukweli kuwa ujira ni kiduchu na watafuta kazi ni wengi.

Hali hiyo imewafanya waajiri kuamua kile wapendacho hasa kwenye mfano na maslahi bora.

Ndiyo maana kila mwaka TUCTA inadai nyongeza ya kiwango cha chini cha mshahara kwa kuamini kuwa huenda kikasaidia kuboresha maisha ya wafanyakazi.

Ni suala ambalo serikali ya awamu ya sita inatakiwa kulifanyiakazi. Kuona kwamba mshahara wa kima cha chini unamwezesha mfanyakazi kuishi badala ya kumweka matatani kwenye madeni yasiyolipika, kufanyakazi akiwa na njaa na hata kushindwa kumudu maisha yake.

### WASIO NA AJIRA

Licha ya kwamba leo ni Mei Mosi maadhimisho yanafanyika wakati idadi ya wafanyakazi wenye ajira rasmi inazidi pungua kila mwaka na huenda maadhimisho hayo yakapoteza nguvu.

Kila leo watu wanalalamika kuhusu jeshi kubwa la vijana wasio na ajira wanaohitimu vyuoni, aidha ukosefu wa hatma kwa vijana wanaomaliza shule na namna ambavyo teknolojia inavyowapokonya kazi.

Mei Mosi imekuwa ni wakati mwingine wa kulalamikia maisha ni magumu kwa wafanyakazi , ni changamoto kwa wanaotafuta ajira, kwa wanaojitolea kupata mafunzo kwa vitendo kazini na kila mmoja ana kilio chake.

### MEI MOSI MPYA

Tanzania ni nchi iliyojaa neema ina ardhi inayofaa kwa kilimo na ufugaji, imesheheni madini, mapori na misitu.

Kadhalika taifa linazo rasilimali za kutosha kama maji ya maziwa, mabwawa, mito, Ukanda wa Bahari Kuu karibu kilomita 1,000 kuanzia Mtwara hadi Tanga.

Vilevile, nchi imejaa madini ya aina mbalimbali vito ikiwamo tanzanite ambayo hupatikana Tanzania pekee, na kuna gesi asilia, ipo helium na madini mengine mengi kama urani ambayo ni muhimu duniani hasa kwenye uzalishaji nishati.

Yote haya yanaashiria kuwa uwekezaji upo na taifa lina fursa nyingi kwa ajili ya kuanzisha ajira rasmi za kutosha na kubadilisha maisha ya Watanzania wasio na kazi.

Hata hivyo uwekezaji na ajira zitakazotokana na rasilimali hizo hazitafanikiwa wala kupunguza malalamiko kila Mei Mosi bila serikali kukomesha, unyanyasaji, uonevu na ukatili katika sehemu za kazi.

Hilo linafanikiwa kwa kusaini, kuridhia na kutekeleza mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) wa C 190, unaosisitiza kazi zenye staha, kuheshimu utu na kuondoa unyanyasaji na dhuluma kazini.

Mkataba huo, unahamasisha waajiri, wafanyakazi na serikali kufanikisha kuwapo na dunia salama ya kazi, isiyo na ukatili wala unyanyasaji kwa wafanyakazi na kuthamini mchango na heshima ya kila mfanyakazi.

Mkataba huo ni dawa ya kuondoa vilio vya kinamama kufanyiwa ukatili kijinsia, kupunjwa mishahara, kunyimwa likizo za uzazi. Si kwao tu, unawatetea pia wanaoishi na ulemavu kupata ajira zenye staha na kulipwa haki na stahiki zao. Aidha, unalenga kuhakikisha kuwa watumishi wanapata ajira zenye staha, wana mikataba ya ajira na kazi zinazoheshimu utu, haki na uhuru wa watu.

Ni vyema serikali ikasaini mkataba huo na kuanza kuutekeleza na hata kuwahamasisha wawekezaji kuutekeleza ili uwekezaji utakaofanyika uwe wa haki na usiochafuliwa na malalamiko ya ukatili na unyanyasaji wa wafanyakazi.

Mkataba wa C190 unasisitiza kuwa kazi za staha na kila mmoja kuheshimiwa utu wake na mchango wake kwenye uzalishaji.

Mkataba huo ni muhimu kwa zama hizi kwa kuwa watu wengi wanafanya kazi lakini wanapunjwa ujira au mshahara, hawawezi kujikimu kwa wamekuwa vibarua na hawana malipo ya uzeeni (pensheni) hasa wanapostaafu au kuacha kazi. Ambacho ndicho kilio cha wafanyakazi na TUCTA kila Mei Mosi.

Kwa Tanzania kuwa na Mei Mosi inayopendeza, salama na yenye tija ni wakati wa serikali na wadau kuona kuwa ni wakati wa kutekeleza kwa vitendo mkataba wa C 190 ili kuwa na taifa lenye dunia salama ya kazi kwa kila mmoja, awe kazini, anayetafuta kazi, anayejitolea , aliyestaafu na kibarua pia.

HABARI KIMATAIFA

# Malkia wa Zulu afariki siku 30 akimrithi mumewe mfalme

**KwaZulu-Natal,** AFRIKA KUSINI

FAMILIA ya kifalme ya Zulu nchini Afrika Kusini imetangaza kifo cha Malkia wake aliyekuwa anaongoza eneo hilo, Shiyiwe Mantfombi Dlamini Zulu, mwezi mmoja tu baada ya kutawazwa kuchukua majukumu ya kifalme.

Malkia Mantfombi, 65, alikuwa kiongozi wa mpito wa kabila la Zulu ambalo ndilo kubwa zaidi nchini Afrika Kusini, baada ya kifo cha mume wake, Mfalme Goodwill Zwelithini.

Waziri Mkuu wa malkia huyo, alisema kifo chake kimeshtua familia ambayo ipo kwenye masikitiko makubwa kwa kumpoteza.

Mrithi wake ambaye atatawala eneo la Wazulu lenye watu milioni 11, bado hajatajwa.

"Ni huzuni na masikitiko makubwa kwamba familia ya Kifalme inatangaza kifo ambacho hakikutarajiwa cha Malkia Shiyiwe Mantfombi Dlamini Zulu wa Wazulu," Mwanamfalme Mangosuthu Buthelezi, waziri wake mkuu alisema kwenye taarifa.

Aliongeza kuwa anataka kuhakikishia watu kwamba hakutakuwa na ombwe la uongozi kwa eneo la Wazulu.

Malkia Mantfombi alilazwa hospitalini wiki moja iliyopita baada ya kuugua ugonjwa ambao haukujulikana, kulingana na vyombo vya habari vya Afrika Kusini.

Alikuwa ameteuliwa kuchukua nafasi hiyo Machi 24, baada ya mume wake, 72, Mfalme Zwethilini, kufariki dunia akiwa hospitalini kwa ugonjwa wa kisukari na matatizo mengine.

Mfalme Zwethilini alikuwa ametawala eneo la Wazulu kwa karibu miaka 50 na kumfanya kuwa mfalme aliyetawala kwa kipindi kirefu zaidi barani Afrika.

Malkia MaDlamini Zulu, alikuwa ameshikilia nafasi ya juu zaidi ya uongozi miongoni mwa wake wa mfalme kwa sababu alitoka familia ya kifalme.

Alikuwa dada ya Mfalme wa Eswatini, Mswati III, nchi pekee Afrika ambayo yote inaendeshwa kwa mfumo wa kifalme.

Malkia MaDlamini Zulu na marehemu muwe wake walijaaliwa watoto wananе, ikiwa ni pamoja na vijana 5 wa kiume.

Kijana wao mkubwa (47), Mwanamfalme Misuzulu, ndiyo mwenye uwezekano mkubwa wa kuchukua uongozi kama mfalme, taarifa zinadokeza.

**BBC**



Raia wa India akipita karibu na matanuri ya kuchomea maiti ya watu waliofariki kwa ugonjwa wa corona. Idadi ya watu wanaopoteza maisha inapanda kila siku kutokana na hospitali kuelemewa na idadi kubwa ya wagonjwa. **(PICHA: AFP)**

# Kenya yerejesha msimamo wake kufunga kambi Kakuma, Dadaab

**Nairobi,** KENYA

KENYA imethibitisha kuwasiliana rasmi na Shirika la kuhudumia Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) na kutaarifu itazifunga kambi za wakimbizi ya Dadaab na Kakuma ifikapo Juni 30, mwakani.

Waziri wa Mambo ya Nje Kenya, Dk. Fred Matiangí alitangaza hayo baada ya kufanya mkutano na Filippo Grandi, mjumbe wa Umoja wa Mataifa (UN), anayeshughulikia wakimbizi.

Dk. Matiangí alisema kuwa timu ya maofisa wa serikali ya Kenya na UNHCR watafuatilia mchakato huo uliopangiwa kuanza Mei 5, mwaka 2022.

Mchakato wa sasa hivi unajumuisha kurejea katika nchi zao kwa hiari au kutoa kibali cha kufanyakazi au cha makazi bila malipo kwa wakimbizi kutoka jamii ya Afrika Mashariki.

Wakati huo huo, Shirika la Kutetea Haki za binadamu la Amnesty International, limefurahishwa na mpango wa kupitiwa tena kwa mpango wa kufunga kambi hizo za wakimbizi.

"Sio kambi za kudumu za wakimbizi au kufungwa kwa haraka kwa kambi hizo au kukiuka kanuni ya kimataifa inayokataza nchi inayopokea wakimbizi kuwarejesha nchini mwao ambako wanaweza kuwa katika hatari ni suluhisho ya hili", UN ilisema.

Katika taarifa iliyotolewa na shirika hilo, ilisema kuwa inaamini serikali ya Kenya na UNHCR itachagua namna nyingine ya kuwahifadhi au kurejea kwa hiari kwa wanaotaka kwa heshima.

Mwezi Machi, mwaka huu, serikali ya Kenya iliiambiaa UN inataka kufunga kambi hizo mbili, ambazo ni makazi kwa wakimbizi 400,000.

Muda mfupi baadae, Shirika la Amnesty International, likajibu kwa kusema kuwa hatua ya kufungwa kwa kambi za Dadaab na Kakuma bila mpangilio unaoheshimu haki za wakimbizi, kutasababisha janga la kibinadamu wakati tayari dunia inakumbana na janga la virusi vya corona.

Kenya imekuwa ikitoa makazi kwa wakimbizi kwa zaidi ya miaka 30 na sasa hivi serikali inasema uwezo wake kuendelea kuwatunza hata kwa kuzingatia viwango vya chini kabisa vya kibinadamu vinavyokubalika, imekuwa tatizo kwa nchi hiyo kuvifikia.

Katibu Mkuu hapa Kenya, Karanja Kibicho, aliongeza kuwa uamuzi wake wa kufunga kambi za Dadaab na Kakuma kufikia Juni 30, 2022 ni kwa maslahi ya raia wa nchi yake.

**BBC**

## Mahujaji 40 wafa kwenye tamasha la kidini Israel

**Jerusalem,** ISRAEL

MAHUJAJI zaidi ya 40 wamepoteza maisha, Kaskazini Mashariki mwa Israel baada ya kukanyagana wakiwa kwenye tamasha la kidini linalofahamika, Lag B'Omer.

Mamlaka inayohusika na majanga ya dharura nchini hapa, haijasema idadi kamili ya watu waliopoteza maisha huku wengine wakiripotiwa kujeruhiwa.

Gazeti la Haaretz, liliripoti kushuhudia miili ya watu 44, huku watu wengine 38 wakikimbizwa hospitalini kupata matibabu baada ya kujeruhiwa.

Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, kupitia ukurasa wake wa Twitter alisema, tukio hilo ni msiba mkubwa na anawaombea wote waliojeruhiwa.

Manusura wa mkanyagano huo walisema, watu walianza kuangushana muda mfupi baada ya kuwapo kwa ujumbe wa dharura kuwa, huenda kukatokea mlipuko wa bomu.

Picha na mikanda ya video iliwaonesha maelfu ya mahujaji wakiwa pamoja kabla ya kila mmoja kuanza kukimbilia usalama wake.

Tamasha la Lag Bomer, huadhimishwa kila mwaka na Wayahudi wenye dini ya Orthodox wanaokusanyika kuwasha moto usiku kucha, wakiomba na kucheza.

**RFI**

## Palestina yaahirisha uchaguzi wa Bunge

**Ramallah,** PALESTINA

RAIS wa Mamlaka ya ndani ya Palestina,

Mahmoud Abbas ametangaza kuwa uchaguzi wa bunge, umeahirishwa.

Rais Abbas alitangaza jana kuwa uchaguzi wa Palestina ulipangwa kufanyika Mei 22, mwaka huu, umeahirishwa kwa muda usiojulikana.

Alitoa tangazo hilo baada ya mkutano na wawakilishi wa makundi kadhaa ya wapalestina mjini Ramallah na kusema, uchaguzi huo hautafanyika hadi serikali yake itakapopata hakikisho kuwa eneo la Jerusalem Mashariki pia litashiriki kupiga kura.

Duru kutoka Palestina zilisema uamuzi huo unatokana na Israel kushindwa kuridhia matakwa ya mamlaka za Palestina za kuruhusu upigaji kura kufanyika pia kwenye eneo hilo la mji wa Jerusalem ambalo linakaliwa kwa mabavu.

Kundi la Hamas ambalo linatawala ukanda wa Gaza ulio sehemu ya mamlaka ya ndani ya Palestina, lilisema halikubaliani na uamuzi wa kuahirishwa kwa uchaguzi huo ambao ungekuwa wa kwanza katika kipindi cha zaidi ya miaka 15.

**DW**

# WFP yaja na mwarobaini wa matatizo ya chakula

**Na Maulid Mmbaga**

KITUO cha Ubunifu cha Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kimeanzisha mradi wa (WFP-X) kwaajili ya kutatua changamoto za chakula.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Mradi kutoka (WFP), Asia Sultani katika maonesho ya mradi huo yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam. Alisema WFP-X inalengo la kuchunguza usalama wa chakula, matatizo yanayohusu lishe, upotevu wa chakula na mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema pia wamebainisha mambo matano ambayo yamekuja na suluhisho la matatizo yanayokumba majiji nchini hasa Jiji la Dar es Salaam.

Alisema miongoni mwa mambo hayo ni mradi wa Forever Food ambao umetengeneza mchanganyiko wa asili unaotokana na utomvu wa miti. Alisema hali hiyo husababisha chakula kisiharibike kwa kuongeza muda wa matumizi wa matunda na mbogamboga kwa zaidi ya siku 20 na kuchochea upandaji wa miti jamii ya mshita.

"Wazo la pili ni Novex ambao ni utengenezaji wa chakula cha mifugo ambacho hugeuza mabaki ya chakula yasiyo na thamani kuwa protini inayotokana na bakteria na inayofaa kulishia mifugo na kupunguza hewa ukaa wakati wa mchakato wa kukiandaa," alisema.

Alitaja jambo la nne kuwa ni NextMeat ambao ni chakula mbadala wa nyama chenye lishe kinachotengenezwa kwa mabuu ya jamii ya nzi weusi yanayovunwa maeneo ya mijini kwa kutumia taka za viumbe hai.

Alitaja lingine kuwa ni Mr. Bin Gas ambao ni mfumo wa utumiaji wa mabaki ya chakula kutengeneza gesi inayotumika katika jamii kama nishati rafiki kwa mazingira.

"Katika mfumo huo tumeandaa mkakati wa kusambaza vifaa maalumu vya kuhifadhia taka majumbani na kwa kila ambaye atatupatia taka hizo kwa wingi atapata huduma ya gesi kwa punguzo la asilimia 50 pia mfumo huo utasaidia kupunguza ugonjwa wa kipindupindu kwa kuwa utatatua tatizo la taka kuzagaa mitaani," alisema. Alitaja la tano kuwa ni Mama Lishe poa ambao ni mnyororo wa mama lishe wanaouza chakula chenye lishe na rafiki kwa mazingira na kwa gharama nafuu ambacho ni rahisi kupatikana kwa wakazi wa Jiji hilo.

Aliongeza kuwa Dar es Salaam imechaguliwa kuwa sehemu ya mradi huo kwasababu ni miongoni mwa majiji yenye idadi kubwa ya watu na yanayokuwa kwa kasi duniani.




Waziri wa Nchi, Ofisi Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akikabidhi tuzo ya mshindi wa pili katika kipengele cha Kilimo kwa Meneja Uhusiano na Biashara wa Kiwanda cha sukari cha Kilombero, Monalisa Juma, katika maadhimisho ya maonesho ya Siku ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi Duniani, katika viwanja vya Nyamagana, jijini Mwanza juzi. Wa (pili kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampuni yakabidhi kituo cha Polisi kwa kijiji

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya OreCorp imekabidhi kituo kipya cha Polisi kwa Kijiji cha Ngoma, kilichopo Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza kilichogharimu Sh. Mil 45.

Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, inayojihusisha na uchimbaji madini ya OreCorp, John Bwana, ndiye alikabidhi kituo hicho kwa Katibu Tawala wa Wilaya Sengerema, Allan Augustine Mhina.

Mhina alipokea msaada huo hivi karibuni kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella kwenye hafla fupi wilayani humo, iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mbunge wa Jimbo la Sengerema, Hamis Tabasamu.

Katibu tawala huyo aliipongeza kampuni ya OreCorp kwa mchango wao huku akieleza kuwa kituo hicho kitawahudumia wakazi wa maeneo yanayozunguka kituo hicho.

Mbwana alitaja miradi mingine kampuni hiyo iliyotekeleza tangu mwaka 2015 kuwa ni pamoja na ukarabati na ujenzi wa madarasa ya shule zilizopo wilayani humo.

Alisema wamekuwa wakitoa msaada wa madawati, mabati, saruji, visima vya maji na upandaji wa miche ya miti ipatayo 11,000.

"Kampuni imetekeleza miradi kadhaa ya kielimu pamoja na kijamii, kwa kuongeza kina cha bwawa la Sotta na uimarishwaji wa miundombinu ya barabara," alisema Mbwana

Alisema makabidhiano hayo yamefanyika wilayani humo, wakati kampuni hiyo ikisubiri kupatiwa leseni ya uchimbaji na kujenga mgodi wa dhahabu wa Nyanzaga, utakaogharimu Sh. Bil 670.

"Kwa kuzingatia kuwa kampuni ya OreCorp bado haijaanza shughuli ya uchimbaji madini, ushiriki wetu kwenye shughuli za maendeleo ya jamii inadhihirisha nia ya dhati ya kampuni yetu katika kushirikiana na wananchi wa Tanzania ili waweze kunufaika na mradi wa Nyanzaga," alisema

Mbwana alifafanua kwamba hadi sasa, OreCorp imelipa kodi kwa serikali zaidi ya Sh.bilioni 10 na kukamilisha miradi 30 ya kuiendeleza jamii kabla ya kuanza uchimbaji wa madini.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Matthew Yates, alisema ujenzi wa kituo hicho cha polisi, uliidhinishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, mwaka jana, baada ya mazungumzo baina ya wakazi wa kijiji cha Sotta na Nyabila, kata ya Igalula na Kamanda wa Polisi wa Mkoa.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Damien Valente, alisema wazo la kujenga kituo hicho lilitolewa na wakazi wenyewe kwa kuwa hawakuwahi kuwa na kituo cha Polisi kwenye eneo lao.

"Tumefurahi kushirikiana na wananchi katika kuleta maendeleo kwa jamii na tutahakikisha kuwa rasilimali walizonazo zinaweza kumnufaisha kila mmoja wao,"alisema

# Mufti aipongeza BancABC kupanua huduma za kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

MUFTI wa Tanzania, Shehe Aboubakary Zubeiry, ameipongeza BancABC kwa kuunga mkono mikakati ya serikali ya kuongeza tija katika sekta ya huduma za fedha na kupanua huduma hizo ili kuwafikia Watanzania walio wengi na ambao hawajafikiwa na huduma za kibenki.

Shehe Zubeiry alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam jana alipozungumza na wateja na wafanyakazi wa BancABC wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake.

"Ninaomba niwapongeze sana nyinyi BancABC Tanzania kwa juhudi zenu kubwa mnazoweka kwenye kupanua huduma zenu ili kuwafikia Watanzania walio wengi na hasa kwenye maeneo ya vijijini.

"Hii ni hatua kubwa sana na ya kupongezwa kwani kadri mnavyoendelea kuwafikia Watanzania wengi ndivyo mnavyozidi kuwafungulia milango ya kujiongeza kiuchumi na hivyo kuunga mkono juhudi za serikali za kuongeza kipato kwa wananchi wake," alisifu.

Shehe Zubeiry aliendelea Akisema: "Nimepata taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji kuwa BancABC pia imekuwa ikishiriki katika utekelezaji wa masuala ya kijamii.

"Mkurugenzi amesema kuwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya wakati wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu (sasa Waziri wa Nchi Ofi ya Rais - TAMISEMI) kwenye kutoa huduma ya bima ya afya kwa watoto yatima, kushirikiana na Taasisi ya Stella Ikupa walikuza uelewa wa huduma jumuishi za kifedha kwa watu wenye ulemavu pamoja na kushirikiana na TAMISEMI katika ujenzi wa vyoo na vyumba vya madarasa ya shule mbalimbali nchini.

"Hii ni ishara tosha kuwa BancABC ni mshirika mzuri katika masuala ya jamii na wanapongeza kwa hilo na kuwaombea kwa Mungu azidi kuwapa nguvu ya kuzidi kufanya zaidi ya hayo."

Awali wakati akimkaribisha Mufti huyo, Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC Tanzania, Imani John, alisema benki hutoa huduma mbalimbali kwa watu binafsi, wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na wateja wakubwa zikiwamo huduma za kuweka fedha pamoja na mikopo wezeshi kwa wateja wa madaraja yote.

"Kwa kipindi ambacho tumekuwa tukitoa huduma, ubunifu wa huduma za BancABC pamoja na mipango yetu madhubuti, imepelekea kutambuliwa na wadau mbalimbali katika sekta ya huduma za kifedha na imetupatia tuzo mbalimbali.

"Na kwa kudhihirisha ubora wa ubunifu wa huduma zetu, BancABC Tanzania ilishinda tuzo ya 'The Most Emerging Bank in East Africa through the Banker Africa - East Africa Awards' yaani tuzo ya benki inayokua kwa haraka Afrika Mashariki kwa Tuzo za Afrika Mashariki ambazo zilifanyika jijini Nairobi kwa miaka miwili mfululizo, 2017 na 2018.

"Hili ni jambo la kujivunia na tunaahidi kuendelea kutoa huduma zenye ubora wa juu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wateja wetu," alisema mkurugenzi huyo.

Aliongeza kuwa BancABC inazo huduma za kadi za malipo ya kabla, ambazo ni maalum kwa wateja kufanya miamala bila ya kuwa na akaunti kwa njia salama na nafuu kwa malipo ya njia ya mtandao na kwenye mashine za malipo (POS) ambazo zimetambuliwa na kupewa tuzo na VISA kwa miaka mitatu mfululizo.

"Tuzo hizo zinazojulikana kama 'Leading in e-Commerce Transactions Award', zinamaanisha kuwa kadi zetu zinaongoza nchini katika malipo ya mtandaoni," alisema.

Alisema kuwa kadi hizo zinapatikana katika sarafu sita tofauti ambazo ni Shilingi ya Tanzania, Dola ya Kimarekani, Randi ya Afrika ya Kusini, Pauni ya Uingereza, Yuro ya Ulaya pamoja na Yuan ya China.

# HADITHI

# Aolewe au afe-4

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake.

Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho.

Inakuwa tafrani. Kijiji hakikaliki. watu wanatafutana. Moto unawaka. Bishada mwenyewe maisha yake yanakuwa hatarini.

Fuatilia kisa hiki ambacho kitakuacha mdomo wazi.

**Na Adam Fungamwango**

**(0716 350534)**




"Kuna siku nilikuwa kisimani, akafika kijana mmoja anaitwa Duma. Yule ambaye alikuwa wa kwanza kuleta barua hapa. Akaniuliza kwa nini umeikataa barua yangu. Nikamwambia siyo lazima. na mwanaume siyo wewe peke yako. Kwani wewe ndiyo una sifa za kuoa tu wengine hawana? Halafu nikamwambia siku nyingine akitaka kuoa kwanza ni vizuri awe anawasiliana na kuolewaji, vinginevyo atakuwa anakosa wachumba kila siku. Wachumba wa sasa siyo kama wa zamani ambao barua zinakuja tu, lakini hawamjui ni nani."

"We mtoto wewe. Una maneno siku hizi."

"Siyo maneno mama kweli, natoka njiani nikakutana na na Mtoka ambaye naye alileta barua yake hapa, akawa ananilaumu kuwa eti nimemkubali Duma wa kijiji cha pili nimemkataa yeye. Sijui nani alimwambia kama nimemkubali Duma. Hapo nikajua kabisa kuwa siku wakikutana itakuwa balaa."

Bi. Fatuma alimtazama binti yake. Naye akatabasamu. Hakika ni mzuri. Alijivunia.

"Lakini binti yangu, hii si inaweza kutuletea balaa hapa kijijini. Yaani hadi najuta kuzaa binti mzuri kama wewe. Kila unapopita kama si salam kutokana na vijana, lakini lawama kutoka kwa wanawake wenzangu na wasichana, wanakuogopa eti utawachukulia wachumba zao na wengine waume zao."

"Wanipishe mimi sina haja na mwanaume."

"Lakini Bishada, yote yataisha kama ukikubali tu kuolewa. Haya yote watu kupigana. Wake wa watu kuwa na hofu na waume zao na wasichana wenzako kuwa na hofu na wanaume zao itaisha."

"Sawa mama, lakini siyo sasa. Mimi sijaamua na sioni hata mwanaume wa kunioa, si kijiji hiki wala vingine vya jirani vinavyotuzunguka."

**********************************

Kiliitishwa kikao cha kijiji. Mwenyekiti Mataulo aliwaita wanakijiji baada ya kupata malalamiko.

Wengi walikusanyika. Mwenyekiti alisimama na kufungua kikao hicho.

"Ndugu wananchi nimewaita hapa kwa ajili kukiweka kijiji chetu sasa. Kwa miezi mitatu sasa kijiji kimeonekana kuwa ma matatizo. Wanakijiji wa Mtakuja wamekuwa hawaelewani tena. Tulikuwa na ushirikiano na vijiji jirani, lakini kwa sasa hakuna tena. Imekuwa ni uhasama," alisema na kuitikiwa "Ndiyoo" na baadhi ya wanawake.

"Na hii yote imetokana na mtu mmoja tu, mnamfahamu wenyewe." "Bishadaaa." Waliitikia tena.

"Ndiyo. Huyu msichana ndiyo ameleta tafrani yote hapa kijijini. Wake wa watu wanamtuhumu kuchukua waume zao na hata wanawake wenye wapenzi nao wanalalamika kuwa anatembea na wapenzi wao. Wanaume na vijana wa kijiji hiki na jirani wamejitokeza kwa wingi nyumbani kwao kwenda kupeleka posa, lakini wamekuwa akitakaa. Na nimeambiwa hataki kwa sababu tayari ameshazoea kutembea na waume za watu." Alisema Mwenyekiti huyo huku akishangiliwa na wanakijiji wengi.

"Kwa sababu malalamiko yamekuwa mengi, basi nimeitisha mkutano huu ili tujue tunalitatua vipi suala hili. Kwa sababu hivi majuzi tu tulikuwa na kikao cha kijiji cha jirani, mwanakijiji mwenzao alipigwa hapa, ikatuletea shida sana."

Vidole vilikuwa vingi. Fursa alipewa dada mmoja ambaye alisimama na kuusalimia umati uliokuwepo.

"Naitwa Prisca, mimi mume wangu hakulala nyumbani siku tatu. Nilipochunguza nikagundua anatembea na huyu msichana. Msichana ni mhuni na hafai kabisa. naomba serikali ya kijiji itoe adhabu kali juu yake." Alisema na kukaa chini.

Prisca, alikuwa mmoja kati ya wanawake walipangwa kutoa maneno ya uongo dhidi ya Biashada.

Watu sita, watatu wakiwa na wanaume na watatu wanawake ambao walitoa maneno ambayo wao wenyewe wanadai ni ushahidi wa matendo maovu ya Bishada.

Hakuna lolote ambalo lilikuwa kweli. Ni kwamba baadhi ya watu kijijini hapo walikuwa na wivu dhidi ya binti huyo aliumbwa na kuumbika.

Alikuwa mwiba kwa baadhi ya wanawake ambao walikuwa na wasiwasi na ndoa zao. Walihisi kuwepo kwake na vile hataki kuolewa, basi anaweza kusababisha ndoa zao kuvunjika au kuyumba kutokana na kumezewa mate na kila mwanaume anayekutana naye.

Wasio na ndoa nao walikuwa na wasiwasi wa kuachwa na wapenzi wao kwa sababu yake.

Kwa wasichana wasiokuwa na wapenzi nao walimchukia kwa sababu wavulana walimsifia Biashada zaidi kuliko wao, hivyo walianza kumtenga hata kutembea naye kwenda kusimani au kuokota kuni.

Wapo wanawake ambao walimfuata na kwa ajili ya kumshawishi awakubali kaka zao, yaani wanaume wengine waliwatumia dada zao ili akubali kuolewa nao, lakini waligonga mwamba.

Wanaume na vijana baadhi yao nao waliingia kwenye kundi la kumchukia msichana huyo kwa sababu pamoja na jitihada zote za kumtongoza, angalau tu kutembea naye, lakini Bishada alikuwa na msimamo thabiti usioyumba.

Achia mbali wale waliopeleka barua za uchumba na zikadunda, ukichanganya, Bishada alikuwa na maadui wengi kuliko alivyodhani.

"Haya wanakijiji, tumepata picha halisi ya msichana huyu jinsi alivyo. Pamoja upole wote kumbe ni mhuni tu. Na hii yote ni kwa sababu hajaolewa. Sasa mimi kama Mwenyekiti. Kabla ya watu kutoa ushuhuda, tulikaa na kamati yangu. Tumeamua kitu kimoja. Tumetoa mwezi mmoja huyu binti awe ameshaolewa au kuposwa ili matatizo yote haya yasiwepo. Vinginevyo mzee Ngoma, mkeo Bi Fatuma tutawafukuza kwenye kijiji hiki." Alisema Mwenyekiti na kufuatiwa na mayowe, vigelegele na makofi.

"Hatufanyi hivi kwa sababu hatumpendi binti au mzee Ngoma, ila tunataka kijiji chetu kirudi kwenye hali ya amani na utulivu. Akiwa ameolewa au kuposwa, hata kama akiwa hapa hapa kijijini, atakuwa tayari yupo kwenye himaya na uangalizi wa mtu, kuliko hivi sasa yupo huru, basi kila mtu macho kwake." Alihitimisha Mwenyekiti na kufunga mkutano huo.

Ni mkutano ambao ulikuwa kwiba kwa familia ya Bishada, lakini ni faraja kwa wale wote ambao wealishawahi kupeleka barua za posa kwa kina Bishada.

Sasa walijua bahati imekuja tena. Walijua safari hii hazitokataliwa tena kama mwanzo. Zaidi ya barua 15 zililetwa nyumbani kwa mzee Ngoma, lakini Bishada alikataa katakata.

Kwa wanawake wao hawakuwa na shida. Walijua Bishada akichumbiwa kwao itakuwa ni nafuu kwenye ndoa zao, au kwa wapenzi wao.

Kazi ilikuwa kwa wanaume. Kila mmoja alijua hata kama Biashada akikubali, lakini barua au posa itakayokubaliwa ni moja tu. Sasa ni nani atakubaliwa?

Mzee Ngoma, mkewe Bi. Fatuma na binti yao Bishada walikuwepo kwenye kikao hicho. Ilikuwa ni aibu kubwa kwao. Mzee Ngoma na mkewe walijua wazi kuwa ulikuwa ni uongo wa wazi ulitungwa.

Wanamfahamu binti yao. Wanafahamu msimamo wake. Pamoja kwa kwamba hawakumuunga mkono kitendo chake cha kukataa wanaume, lakini walisimama upande wake kupinga uongo wote juu yake.

Bishada alilia wiki nzima. Alikaa ndani tu. Hata kula alikataa. Alikuwa akibembelezwa na mama yake na shoga yake Mariam.

***Itaendelea Jumamosi***



# KANE
## ASEMA ANATAKA MATAJI, SI TUZO

**LONDON, England**

HARRY Kane amesema kushinda tuzo binafsi ni "nzuri sana" lakini yeye kipaumbele chake kikubwa ni kushinda mataji wakati huu uvumi ukitawala juu ya majaliwa yake pale Tottenham Hotspur.

Nahodha huyo wa England alitajwa kuwa mchezaji bora wa kwanza wa Ligi Kuu England, Jumanne katika tunzo za wachezaji.

Kane ameendelea kuwa kwenye kiwango cha juu kwa klabu na nchini yake, lakini straika huyo alikuwa kwenye wakati wa huzuni zaidi baada ya Manchester City kuifunga Spurs 1-0 kwenye fainali ya kombe la EFL, Jumapili.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka kwenye klabu yake huyo ya utotoni na amesema atafikiria kuhusu majaliwa yake baada ya michuano ya Euro 2020.

"Tuzo binafsi ni nzuri, ni mafanikio ya kuvutia," alisema katika mahojiano na Evening Standard.

"Nikiangalia nyuma katika kipindi changu cha uchezaji, naona kama kuna vitu bad sijaweza kufanikiwa.

"Malengo yangu kwa sasa kama mchezaji ni kushinda mataji mengi zaidi kadili inavyowezekana.

"Nataka kuwa kwenye zawadi kubwa na hizo ni mataji kwa timu na sio tuzo binafsi tu."

## LINGARD AKATAA KURUDI MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

JESSE Lingard amebainisha kwamba, hana mpango wa kurejea katika timu yake ya Manchester United.

Lingard kwa sasa anakipiga West Ham kwa mkopo tangu Januari mwaka huu, akitokea Man United na akiwa kwenye kiwango kizuri.


Ripoti zinaeleza kuwa Lingard anampango wa kuomba kuondoka moja kwa moja ifikapo mwishoni mwa msimu huu.

Tangu amejiunga na West Ham amefanikiwa kufunga mabao tisa katika mechi 11 na amesaliwa na mkataba wa mwaka mmoja ndani ya United.

West Ham wanataka kumsajili nyota huyo moja kwa moja huku ada ya kumng'oa nyota huyo ni kiasi cha pauni 15m. Kocha Ole Gunnar Solskjaer yupo tayari kumpokea nyota huyo kikosini kwake na alikuja kupambania nafasi yake.

Inaelezwa kuwa Lingard sasa ameamua kuachana na klabu yake hiyo ya utotoni, kutokana na Solskjaer kutokuwa na imani naye.

Mbali na West Ham, klabu kama Arsenal, Inter Milan na Paris Saint Germain zimekuwa zikimtolea macho Lingard kuelekea msimu ujao.



## KROENKE AGOMA KUIUZA ARSENAL

**LONDON, England**

LICHA ya maadamano makali yanayofanywa na mashabiki wa Arsenal kumuhitaji mmiliki wa hisa zote wa timu hiyo, Stan Kroenke kuuza hisa zake na kuachia madaraka, bilionea huyo amekataa kufanya hivyo.

Mashabiki wa Arsenal walionekana kuandamana kuanzia wiki iliyopita kumhitaji mmiliki huyo aondoke kutokana na mwenendo mbaya wa timu yao.

Mara baada ya mashabiki kuonyesha hasira zao kwa kutembea makundi kwa makundi karibu na lilipo dimba la Fly Emirates, ilitoka taarifa kwamba mwanzilishi wa kampuni ya Spotify, Daniel Ek yupo tayari kuinunua timu hiyo kwa pauni bilioni 2.5, lakini Kreonke bado anaonekana kuwa mbishi. Bilionea huyo kutoka Marekani kwa sasa ndio mmiliki pekee wa timu hiyo akishikilia hisa zote baada ya miaka mitatu iliyopita kununua hisa za mshirika mwenzake Alisher Usmanov.

Kroenke alitoa taarifa iliyoeleza kwamba:"katika siku za hivi karibuni, kumekuwa na uzushi katika vyombo mbalimbali vya habari kuwa tunaweza kukubali kuuza hisa zetu

"Tutabakiwa na asilima zetu 100 na hatuna mpango wa kuuza hata asilimia moja ya hisa, kwanza hakuna ofa yoyote tuliyopokea na hata tukipokea hatuna mpango wa kuikubali.

"Lengo letu sisi kama Arsenal ni kushinda mataji makubwa na kuboresha kikosi chetu."alisema.




# ARTETA: ARSENAL HAIKUCHEZA VIZURI

**MADRID, Hispania**

MIKEL Arteta amekubali kipigo cha mabao 2-1 kuwa yalikuwa matokeo bora baada ya Arsenal kuchapwa na Villarreal kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya ligi ya Europa, Alhamis.

Manu Trigueros na Raul Albiol walifunga mabao kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha wa zamani wa Arsenal, Unai Emery, kabla ya Nikolas Pepe kuwafungia washikabunduki hao.

Arsenal walikosa nafasi nzuri ya kusawazisha baada ya Pierre-Emerick Aubameyang kushindwa kufunga wakati alipobaki yeye na golikipa, Geronimo Rulli.

"Hatukutaka kuja hapa na kupoteza, lakini baada ya kufungwa 2-0 na kubakiwa na wachezaji 10 uwanjani na sisi kupata bao moja, unatakiwa kukubali matokeo," alisema Arteta akiiambia BT Sport.

"Kama unapoteza, haya ni matokeo mazuri ambayo tulitakiwa kuwa nayo. Lakini kulikuwa na vipindi viwili tofauti."

Alipoulizwa nini kilimfanya kubadilisha timu yake baada ya kipindi cha kwanza, alijibu: "Tulianza kuwa sisi. Katika kipindi cha kwanza, kulikuwa na nyakati nyingi ambazo hatukuwa sisi.

"Hatukuwa na muunganiko, tulishindwa kumiliki mpira, hatukuwa kwenye kiwango chetu."

## POCHETTINO AUMIZWA NA KIPIGO CHA MAN CITY

**PARIS, Ufaransa**

MAURICIO Pochettino amesema ni ngumu kukubali kuwa Paris Saint-Germain imepoteza kwa Manchester City kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya.

City iliondoka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya PSG kwenye mchezo huo wa kwanza Jumatano mjini Paris. Nahodha wa PSG, Marquinhos alianza kwa kufunga bao la uongozi dakika ya 15 kwa kichwa, kabla ya City kurudi mchezoni kusawazisha na kupata bao la ushindi.

Alianza Kevin De Bruyne kusawazisha, kabla ya Riyad Mahrez kufunga la ushindi kwa mkwaju wa adhabu ndogo dakika saba baadae, huku PSG wakimaliza mchezo wakiwa na wachezaji 10 uwanjani baada ya Idrissa Gueye kuoneshwa kadi nyekundu dakika ya 77.

Miamba hao wa Ligue 1 wana mlima mkubwa wa kufuzu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya kwa msimu wa pili mfululizo, wakati Pochettino akilaumu namna walivyoshindwa kupata ushindi.

"Kulikuwa na nyakati mbili tofauti. Kipindi cha kwanza tulifanya vizuri. Tulitengeneza nafasi na tulistahili kushinda, lakini kipindi cha pili wao walikuwa bora zaidi kuliko sisi," alisema Pochettino akiiambia BT Sport.

"Mabao mawili yalikuwa ni ajali, lakini walitengeneza nafasi nyingi zaidi kuliko sisi. Mwisho wa siku ilikuwa kila timu imecheza vizuri kipindi kimoja.

"Tumekatishwa tamaa na mabao mawili. Ni ngumu kukubali kwamba hili linatokea kwenye nusu fainali, kwa hakika inaumiza. Kipindi cha pili walikuwa kwenye ubora zaidi.

"Ilikuwa ngumu kwa upande wetu kwenda na kasi yao. Ni ngumu, walikuwa vizuri zaidi. Ilikuwa ngumu kwa upande wetu kupata mpira."

# UNITED KUMNG'OA DEMBELE KWA EURO MIL 50

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa ipo tayari kutoa euro milioni 50 kwa ajili ya kupata saini ya mchezaji wa Barcelona, Ousman Dembele katika malengo ya kuboresha eneo la ushambuliaji.

Kwa mujibu wa gazeti moja la nchini Hispania la Fichajes, Barcelona wameweka dau la euro milioni 50 kwa mchezaji huyo kama klabu hiyo ya Uingereza watahitaji huduma ya Dembele.

United wamekuwa mawindoni kutafuta mshambuliaji wa kudumu wa klabu hiyo baada ya mkataba wa mchezaji wao wa sasa Edinson Cavani kuelekea ukingoni huku mchezaji huyo akisuasua kuongeza mkataba.

Mchezaji huyo wa Ufaransa amekuwa na msimu mzuri katika kikosi cha kocha Donald Koeman cha msimu huu, akifunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho 4 kwenye michezo 39 ya mashindano yote.

Kutokana na hali mbaya ya uchumi ya Barcelona na mchezo usiokuwa bora wa mara kwa mara, wanalazimika kumuuza mchezaji huyo ili kuboresha kikosi chao kwa msimu ujao.

United wamekuwa wakitafuta saini ya mchezaji huyo wa Barcelona toka msimu uliopita bila mafanikio, huku ule usajili mkubwa wa Jadon Sancho wa Dortmund nao ukionekana kutoonesha mafanikio yoyote.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: KAZI BADO HAIJAISHA

●●●Asema wamejipanga vizuri kwa mchezo wa pili kwa Roma na...

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amesema "kazi bado" haijaisha, baada ya Manchester United kuifumua AS Roma mabao 6-2 kwenye nusu fainali ya kwanza ya Ligi ya Europa.

Bruno Fernandes aliwapa mashetani wekundu bao la uongozi wa mapema pale katika dimba la Old Trafford Alhamisi, lakini penalti ya Lorenzo Pellegrini ikasawazisha bao hilo na Edin Dzeko akaifanya AS Roma kuwa mbele kwa 2-1 kipindi cha kwanza.

Roma waliwapoteza wachezaji watatu kwa majeruhi kipindi cha kwanza akiwamo golikipa Pau Lopez na kujikuta wakikumbana na kichapo hicho kutoka kwa United.

Mabao mawili kutoka kwa Edinson Cavani yakawaweka mbele tena miamba hao wa Ligi Kuu England kabla ya Fernandes kufunga la nne kwa mkwaju wa penalti.

Paul Pogba na Mason Greenwood kila mmoja akafunga moja na kuwafanya mashetani wekundu hao kuondoka na ushindi wa mabao 6-2.

Man United sasa wametanguliza mguu mmoja kwenye fainali itakayowakutanisha kati ya Villarreal au Arsenal kule Gdansk, Mei 26 mwaka huu.

Man United iliweka rekodi ya kufunga mabao mengi zaidi kwenye mashindano ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu ilipofunga mabao saba dhidi ya hao hao Roma, Aprili 2007.

Pia imekuwa timu ya kwanza kufunga mabao mengi kwenye hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu Real Madrid ilipofanya hivyo kwenye kombe la Ulaya Mei, mwaka 1964.

Lakini bado Solskjaer amesema kuwa kazi haijamalizika na wanatakiwa kucheza kwa uangalifu kwenye mchezo wa pili kule kwenye uwanja wa Olimpico, Alhamisi ijayo.

Solskjaer aliiambia BT Sport: "Sidhani kama kazi imeisha, ingawa kazi nzuri imefanyika. Tulifanya kazi nzuri na tunajua kwamba wana ubora.

"Walifunga mabao mawili kutokana na nafasi tuliyowapa. Hawakuwa na nafasi nyingi kama ilivyokuwa dhidi ya Ajax. Kipindi cha pili kilikuwa kizuri sana."

Solskjaer pia aliridhishwa na namna kikosi chake hicho kilivyoweza kutulia katika kipindi cha kwanza.

## KWA UFUPI

**SUAREZ AMSHAURI MESSI**
MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Luis Suarez, aliyeondoka Barcelona kujiunga na Atletico Madrid msimu uliopita, amemtaka Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kubakia Nou Camp. **(TV3, via Sport)**

**VILLA WAMTAKA ABRAHAM**
ASTON Villa ipo kwenye nafasi ya kuwania kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23. **(Mirror)**

**DORTMUND YAMTAKA WHITE**
KLABU ya Borussia Dortmund imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mlinzi, Ben White, mwenye umri wa miaka 23, huku Paris St-Germain, Manchester United na Arsenal zikimnyatia. **(Sun)**

**ALABA SAFI MADRID**
REAL Madrid iko tayari kutangaza kumsajili mlinzi wa Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, kwa uhamisho wa bure kutoka Bayern Munich ambako mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. **(Mundo Deportivo - in Spanish)**

**SPURS YAMTAKA HAG**
KLABU ya Tottenham Hotspur, inataka kuzungumza na Erik ten Hag kuhusu kuwa kocha wao mpya baada ya Jose Mourinho kutimuliwa. Hag mwenye umri wa miaka 51, yuko tayari kuchukua jukumu hilo jipya baada ya kuwa kocha wa Ajax kwa miaka minne. **(Guardian)**

**LUKAKU HAUZWI**
INTER Milan imeieleza Manchester City kuwa haipo tayari kusikiliza ofa yoyote kwa ajili ya mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27. **(Calciomercato)**

**LEICESTER YAMUWANIA GOSENS**
KLABU ya Leicester inawania kumsajili mlinzi wa Atalanta na Ujerumani, Robin Gosens, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa itafanikiwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. **(Tuttomercatoweb, via Team Talk)**

**YOUNG KUSAJILIWA JUMLA**
INTER Milan inafikiria kutoa ofa yake ya mkataba mpya kwa mlinzi wa England, Ashley Young ikiwa itashinda kombe la Serie A wikiendi hii. **(Mirror)**

**EVERTON YAMTAKA HEE-CHAN**
EVERTON ni miongoni mwa klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zinazomsaka mshambuliaji wa RB Leipzig raia wa Kore Kusini, Hwang Heechan mwenye umri wa miaka 25. **(Goal)**

**SAKA ALICHAGUA ARSENAL**
KIUNGO wa Arsenal, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 19, amesema hakusita kutia saini kwa washikabunduki hao, licha ya kutakiwa na Borussia Dortmund na Liverpool. **(ESPN)**

**LEMINA AGOMBEWA**
TIMU za West Ham na Newcastle zimeonesha nia ya kutaka kumsajili, Mario Lemina wa Southampton. Kiungo huyo wa kati raia wa Gabon mwenye umri wa miaka 27, sasa hivi yuko Fulham kwa mkopo na anapatika kwa pauni milioni 7. **(Guardian)**

HABARI MICHEZO

# SIMBA YAMALIZA NA MAJEMBE YAKE YOTE

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umemalizana na majembe yao yote kwa kuwaongezea mikataba wakiwemo mabeki, Erasto Nyoni na Kennedy Juma ambao wameongeza miaka miwili kukitumikia kikosi hicho.

Awali Simba iliwawaongezea mikataba mipya wachezaji watatu, Mohammed Hussein `Tshabalala`, Shomari Kapombe na John Bocco, ambapo mikataba yao ya awali ilikuwa inafikia mwisho msimu huu wa 2020/21.

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili, viongozi walikuwa na mazungumzo na nyota wao ambao mikataba yao inafikia ukingoni na kukubaliana akiwamo Kennedy na Nyoni ambao jana (juzi) wamesaini mkataba mipya.

Mmoja wa viongozi wa Simba ambaye hakutaka kutajwa jina alisema wako makini katika suala la kuhakikisha wanamalizana na nyota wao wote, ambao mikataba yao inafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu na kuwaongezea kwa mujibu wa matakwa ya benchji la ufundi linaloongozwa na kocha mkuu, Didier Gomes.

"Hatufanyi mambo kwa kukurupuka, kila jambo linafanywa kwa utaratibu wake, sasa tumeshamaliza na baadhi ya nyota mikataba yao iko ukingoni, lakini pia hatuajaishia hapo tunaendelea na sasa tuko katika hatua ya mwisho kumalizana na beki wetu, Gadiel Michael.

"Gadiel mazungumzo yanaendelea, bado tunaendelea katika suala la maslahi ikiwamo dau la usajili ambalo anahitaji milioni 90 na mezani kuna milioni 80, hivyo nina imani kila kitu kitaenda sawa kwa nyota huyo na wengine akiwamo kipa, Beno (Kakolanya), Mkude (Jonas) na Mzamiru (Yassin)," alisema kigogo huyo.

Alipotafutwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu alisema uongozi wa Simba unafanya majukumu yao kwa utaratibu ikiwamo suala la mikataba ya wachezaji ambao liko ukingoni.

Alisema uongozi wa Simba chini ya Mtendaji Mkuu, Barbara Gonzalez, unaendelea na harakati za kuwaongeza mikataba nyota ambao kandarasi zao zinaelekea ukingoni.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kisutu na Boma, wakichuana katika mchezo wa netiboli wakati wa maandalizi ya mashindano ya Umoja wa Michezo kwa Shule za Msingi (UMISHUMTA) katika viwanja vya michezo Jakaya Kikwete, Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Azam yapania kubeba kombe la FA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho, FA, uongozi wa Azam FC umesema malengo yao sasa ni kuhakikisha wanatwaa ubingwa huo.

Azam juzi ilifanikiwa kutinga robo fainali baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, dhidi ya Polisi Tanzania katika mchezo wa hatua ya 16 uliopigwa uwanja wa Azam Complex, Chamanzi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Azam, Zakaria Thabiti `Zaka za Kazi`, alisema mchezo dhidi ya Polisi Tanzania wamemaliza salama na hakuna majeruhi na sasa wanajipanga kwa hatua ya robo fainali.

Alisema malengo yao msimu huu ni kushinda mataji matatu, wamekosa kombe la Mapinduzi, huku wakiendelea kupambania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania na asilimia kubwa kuandaa silaha zake kuhakikisha wananyakuwa FA.

"Tumekosa Mapinduzi, katika ligi kuu ndio hivyo tunapambana mdogo mdogo, ila kwenye FA lazima tuwe makini kuchukuwa kombe hilo na kufanikiwa kwenda kushiriki michuano ya kimataifa kwa msimu ujao."

"Matumaini ni makubwa ya kufikia malengo yetu hayo kwa sababu ya maandalizi tunayofanya na sasa tuna subiri droo ili kumjua mpinzani wetu tutakayecheza naye hatua ya robo fainali," alisema Zaka.

Alisema licha ya kuandaa silaha zake kwa ajili ya kumsubiri mpinzani wao lakini pia watapambana hadi hatua za mwisho kwenye michezo yao ya ligi kuu kutafuta pointi tatu muhimu iwe nyumbani na ugenini kwa lengo la kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo wa ligi hiyo.

## Polisi wajipanga kwa lala salama

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Hamsini Malale, amesema baada ya kuondolewa kwenye mashindano ya kombe la Shirikisho FA, sasa nguvu zao wanazielekeza katika michezo ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Malale alisema wameshindwa kusonga mbele kwenye michuano ya FA kwa kukubali kupoteza mbele ya Azam FC, lakini bado yuko katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi na kupigania timu hiyo kuendelea kupata matokeo mazuri.

Alisema kuna ushindani mkubwa kwenye ligi kipindi cha lala salama na kuhakikisha wachezaji wake wanajituma na kujitoa kwa ajili ya kutafuta pointi muhimu katika michezo ya ligi hiyo ili kuendelea kubaki kwa msimu unaofuata.

"Tumekubali kupoteza dhidi ya Azam FC na kuondolewa kwenye michuano ya FA, ila bado tuna kibarua kingine kwenye ligi na kuhakikisha tunashinda mechi zetu na kutuweka kwenye nafasi nzuri kwenye msimamo na kujiimarisha kuendelea kuwapo katika ligi kwa msimu unaofuata," alisema Malale.

## Mbeya kwanza yafunguka kuhamia Pwani

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya Kwanza, ambayo imekuwa timu ya kwanza kupanda Ligi Kuu msimu huu, imetamba kuwa itafanya vema kwenye ligi msimu wa 2021/22, huku ikifunguka ni kwa nini iliamua kuhamia kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Meneja wa timu hiyo, Emmanuel Gabriel alisema kuwa kupanda kwa timu hiyo ni kutokana na kuwa na kikosi bora, pamoja na ushirikiano kati ya wachezaji, benchi la ufundi na viongozi.

Alipoulizwa kama kupanda kwao Ligi Kuu kunahusisha na kuhamia Pwani, alisema kuwa inawezekana kwa sababu walipokuwa wakichezea mkoani Mbeya kwa misimu miwili walishindwa kupanda kwa pointi chache.

"Siyo kwa asilimia zote, lakini inawekana kwa sababu tulipokuwa nyumbani Mbeya kwa misimu miwili tulishindwa kupanda kwa pointi chache. Lakini inawezekana kwa sababu kule kuna timu nyingi za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza, ambazo tulikuwa tunatumia uwanja mmoja, acha Mbeya City, kuna Boma FC pia ambayo ipo Daraja la Kwanza, ukichanganya na zingine zinasababisha uwanja kuwa na mechi nyingi. Na hii ndiyo imesababisha tuhamie huku Pwani na kwa bahati kubwa tumepanda," alisema Gabriel, straika wa zamani wa Simba.

# Michezo

Jumamosi Mei 1, 2021

Nipashe




SOLSKJAER: KAZI BADO HAIJAISHA

HABARI UK 22




Kiungo wa Manchester United, Paul Pogba (kushoto), akifunga bao dhidi ya AS Roma kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Europa baina ya timu hizo juzi Alhamis, kwenye uwanja wa Old Trafford. Man United ilishinda mabao 6-2. **PICHA: MATANDAO**

# Ni Simba vs Kaizer Chiefs Ligi ya Mabingwa Afrika

● ● ● Mechi ya kwanza kuanzia ugenini Mei 14 au 15 kabla ya ...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa kundi A kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, itaanzia ugenini nchini Afrika Kusini dhidi ya Kaizer Chiefs, ikiwa ni mechi ya kwanza ya robo fainali.

Kwa mujibu wa droo iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), jiji Cairo nchini Misri, Simba imepangwa kucheza na Wasauzi hao, ikizikwepa timu za MC Alger na CR Belouizdad ya Algeria.

Simba imepangwa kucheza Mei 14 au 15 mwaka huu kwenye Uwanja wa FNB nchini Afrika Kusini na mechi ya marudiano itakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Mei 21 au 22.

Ratiba hiyo inaonyesha iwapo Simba ikifanikiwa kupita hatua ya robo fainali na kwenda nusu, itacheza na mshindi kati ya MC Alger ya Algeria na Wydad Casablanca ya Morocco.

Ina maana kuwa Simba imezikwepa timu ngumu za Al Ahly ya Misri na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ambazo zinapewa nafasi kubwa ya kutwaa Ubingwa wa Afrika, yoyote ikatakayoshinda hapo.

Simba iliongoza kwenye Kundi A ikiwa na pointi 13, ikishinda mechi nne, sare moja na kupoteza moja, ikipachika mabao tisa na kufungwa mawili.

Wawakilishi hao wa Tanzania waliwafunga AS Vita mara mbili, Al Ahly mara moja na Al Merrikh mara moja, ikifungwa na Al Ahly ugenini na sare dhidi ya Al Merrikh ugenini.

Kwa mujibu wa ratiba nzima ilivyopangwa ni kwamba mabingwa watetezi Al Ahly ya Misri imepangwa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, mechi itakayoanzia jijini Cairo, MC Alger ya Algeria ikienda ugenini kuifuata Wydad Casablanca, timu ambayo anachezea Mtanzania, Simon Msuva.

Timu nyingine ya Algeria, CR Belouizad nayo itakwenda ugenini nchini Tunisia kucheza dhidi ya Esperance ya huko, kabla ya kurudiana wiki moja baadaye.

Wakati ikiwa hivyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, kwenye Kombe la Shirikisho ambalo wawakilishi wa Tanzania kwenye Namungo wakiwa wameshatolewa, timu ya Orlando Pitates ya Afrika Kusini itacheza dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco, Coton Sport FC ya Cameroon itakuwa mgeni wa ASC Jaraaf ya Senegal, Pyramids ya Misri ikicheza dhidi ya Enyimba ya Nigeria na CS Sfaxien ya Tunisia itakipiga dhidi ya JS ya Algeria.

## YANGA YATINGA ROBO FAINALI FA

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na raia wa Burkina Faso, Yacouba Songne dakika ya 54 lililiipa Yanga ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga na kupeleka kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la FA.

Straika huyo aliwatoroka mabeki wawili wa Prisons na kuiwahi pasi ya kupenyezwa kutoka kwa Mrundi Saido Ntibazonkiza, kabla ya kumchambua kirahisi kipa Jerehiah Kisubi.

Yacouba alifunga bao hilo baada ya kukosa mabao mawili ya wazi kipindi cha kwanza.

Moja akiruka juu na kupiga kichwa akiwa na lango tupu, lakini mpira ulitoka nje sentimeta cheche, nafasi nyingine ikiwa ni dakika ya 45 alipopata nafasi nyingine, lakini badala ya kupiga shuti, alipiga krosi ambayo Ditram Nchimbi aliukosa mpira na ukatoka nje.

Kipindi cha kwanza timu zote zilionekana kucheza taratibu, huku zikishambuliana kwa zamu, lakini Yanga ikiwa na mashabulizi ya hatari zaidi.

Baada ya kufungwa bao hilo, Prisons ilionekana kuamka na kwenye dakika ya 65, mabeki wa Yanga waliokoa mpira kizembe golini kwao na kumkuta nahodha Benjamin Asukile ambaye alipiga shuti kali umbali wa mita 30, lililodakwa kwa ustadi na kipa Metacha Mnata ambaye jana alirejea langoni baada ya kutoonekana tangu Machi 7, alikaa langoni dhidi ya Polisi Tanzania, timu yake ikitoka sare ya bao 1-1.

Dakika ya 77, mechi ilitaka kuingia dosari baada ya Jeremiah Juma aliyekuwa akikimbizana na Lamine Moro kuonekana kuanguka kwenye eneo la hatari na mwamuzi kushindwa kutoa penalti, hali iliyosababisha wachezaji na benchi la ufundi la Prisons kuhamaki.

Ni kama vile Prisons walitolewa kwenye mchezo baada ya tukio hilo na kuanza kucheza kwa hasira, huku Yanga wakionekana kutawala mechi.

Yanga imeweka rekodi ya kuingia tena hatua ya robo fainali kama msimu uliopita ilipoichapa kahera Sugar mabao 2-1, kabla ya kutolewa hatua ya nusu fainali Julai 12 mwaka jana ilipochabangwa mabao 4-1 dhidi ya Simba ambao ndiyo mabingwa watetezi wa michuano hiyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002